Nipashe
Ijumaa Juni 30, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581357
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Uhaba** wa dola wakwaza ununuzi, malipo ya tumbaku

UKURASA 3



**Migogoro** ya ardhi Dodoma yashtua, mkakati wasukwa

UKURASA 4


Anayeikwaza NEMC anakwaza maisha yake

BUFE

Siku wakazi Nyamagana walivyochoshwa na kero barabara, waingia kazini kujitengenezea

UCHUMI

Uchumi Buluu unaowaunganisha 'kuwatoa' wanawake na vijana wa Pemba na Tanga

•Wawekewa mtaji mezani waianze safari

UKURASA 11

BAKWATA NA BANDARI:

# Wasikilizeni, wapeni majibu wananchi

• **Waziri** Mkuu atoa msimamo wa serikali...*Uk. 2*



Baadhi ya waumini wa Dini ya Kiislamu wakishiriki swala ya Eid Al Adha katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana.Picha zaidi uk.18 **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mbaroni tuhuma kumwagia tindikali mke na mwanawe

UKURASA 3

UKURASA 3 & 17

## Samia, Mwinyi wasisitiza amani, kutogawanyika



**MICHEZO** **YANGA YAKANA KUFUNGIWA USAJILI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# BAKWATA: Wasikilizeni, waelimisheni, wapeni majibu wananchi Bandari

**Na Romana Mallya**




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwahutubia waumini wa dini ya Kiislamu, alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika swala na Baraza la Eid Al Adha Kitaifa, katika Msikiti wa Mfalme wa Morocco Muhammad VI, Kinondoni Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), limeishauri serikali ipokee mawazo ya wananchi kuhusu uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam kisha kuyafanyia kazi haraka na kutoa majibu sahihi kwa wananchi katika maeneo yanayotiliwa shaka.

Katibu Mkuu wa BAKWATA, Alhaj Nuhu Mruma, katika salamu zake za Baraza la Eid El-Adh'haa lililofanyika katika Msikiti wa Mfalme Mohammed wa VI wa Morocco ulioko Kinondoni, Dar es Salaam jana, alisema serikali inapaswa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu suala hilo.

Kauli hiyo yenye sauti ya kitaifa, imetolewa ikiwa ni siku moja baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa katika hotuba ya kuahirisha mkutano wa Bunge juzi, alisisitiza mantiki kwa umma wa Watanzania kwamba Bandari isiligawe Taifa.

Vilevile, Waziri Mkuu akiwa sehemu ya hadhira ya tukio la jana la BAKWATA, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, akalitolea ufafanuzi, akirejea kauli yake ya juzi kwamba bandari isiwagawe Watanzania kwa kuwa serikali ni sikivu.

Katika salamu zake, Alhaj Mruma alisema BAKWATA inampongeza Rais Samia kwa juhudi anayoifanya katika kuinua uchumi wa nchi, hasa kwa kukaribisha sekta binafsi na wawekezaji kutoka nje kuwekeza ili kukuza uchumi.

"Pamoja na dhamira hiyo njema kwa nchi yetu katika sekta ya uwekezaji, hivi karibuni umezuka mjadala mpana kuhusiana na makubaliano ya ushirikiano na kuendeleza Bandari Tanzania na Dubai," alisema.

Alhaj Mruma alisema suala hilo la bandari awali lilizua taharuki kwa wananchi wengi ambao hawakuwa na taarifa sahihi za mradi huo. Akasifu viongozi wa serikali kwa namna ambavyo wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mradi huo na faida zake.

"Kwa maelezo ya awali ya wataalamu wetu, mradi huu ni wa kuongeza ufanisi katika bandari zetu na unapaswa kuungwa mkono na kila mpenda maendeleo ya nchi yetu," alisema.

Kiongozi huyo wa BAKWATA alisema wito wao kwa serikali ni ipokee mawazo ya wananchi na kuyafanyia kazi haraka ikiwa ni pamoja na kutoa majibu sahihi kwa wananchi kwenye maeneo yanayotiliwa shaka.

Pia alisema serikali ichukue jukumu la kutoa elimu kwa wananchi na kuwajengea ufahamu mzuri kuhusu faida za mkataba au ushirikiano huo.

"Kipekee tumpongeze Rais wetu kwa kuendesha serikali kwa uwazi mkubwa hata kufikia hatua mkataba mkubwa kama huu kujadiliwa hadharani na wananchi.

**SHIDA MAADILI**

Kuhusu tatizo la mmomonyoko wa maadili, Alhaj Mruma alisema nchi kwa sasa imekumbwa na wimbi hilo kutokana na kupandikizwa tamaduni za kigeni, yakiwamo mapenzi ya jinsia moja.

"BAKWATA tunaendelea kulaani sana na kukemea vitendo hivyo. Tunaendelea kusisitiza kuhusu malezi mema ya vijana wetu ili kuwakuza katika maadili mema.

"Malezi haya mema yataliondoa Taifa letu katika wimbi kubwa la mmomonyoko wa maadili.

Tunawaomba sana wazazi wote kusimamia misingi imara katika familia zao ambazo ndiyo chimbuko la tabia njema linalotokana na malezi ya familia," alisema.

Aliongeza kuwa uislamu kwa ujumla umehimiza tabia njema na umetoa wito katika kuweka Waislamu kuhusu tabia njema na kuziendeleza nafsi zao na umezingatia imani ya mtu kutokana na mema yake, nafsi yake na uislamu wake kutokana na uzuri wa tabia yake.

**SHURA YA MAIMAMU**

Shura ya Maimamu Tanzania nalo haliko mbali na sakata hilo, likitaka mjadala ujikite katika kuongeza ufanisi wa bandari ili kuongeza mapato ya serikali na fedha za kigeni.

Katika tamko lao lililotolewa jana na kutiwa saini na Amiri Shaaban Ibrahim, lilisisitiza "Kama tulivyosema huko nyuma, mjadala wetu ujikite zaidi katika kuongeza ufanisi wa bandari yetu ili kuongeza mapato ya serikali na fedha za kigeni.

"Tuungane na Wanzania wanaosema tuboreshe mkataba wa bandari tusonge mbele kwa maslahi ya taifa letu," sehemu ya tamko hilo inasomeka.

**BANDARI ISITUGAWE**

Katika hotuba yake jana, Waziri Mkuu Majaliwa alisisitiza: "Mjadala unaoendelea kuhusu Bandari ya Dar es Salaam usitugawe Watanzania. Usipelekee tukasambaratika.

Tusitumie nafasi hiyo kutugawa kiitikadi, kidini au kisiasa. Sisi ni wamoja na jambo letu ni moja. Serikali yenu sikivu, itaratibu haya."

Alisema serikali inapokea maoni na ushauri kutoka kwa wadau na ina nia njema kuhusu suala hilo na ndiyo maana iliiliweka hadharani.

"Ninatambua kuna watu wana hofu na umiliki wa bandari, ajira, ardhi na usalama wa Taifa lakini tusisahau kuwa TICTS wamekuwapo pale kwa miaka zaidi ya 22.

"Niwatoe hofu Watanzania kuwa malengo yetu ni kuboresha uchumi wa Tanzania. Tunataka watumiaji (wa bandari) waliohama warejee," alisema.

Waziri Mkuu alikumbusha kwamba Tanzania imezungukwa na nchi nane ambazo hazina bandari na zinategemea Bandari ya Dar es Salaam kupitishia mizigo.

"Kwa hiyo, Bandari ya Dar es Salaam ni kitovu cha uchumi. Mwekezaji huyu ana uzoefu mkubwa na teknolojia ya hali ya juu katika uendeshaji shughuli za bandari katika nchi 68. "Sisi pia tunatamani kufanya vizuri kama yeye alivyofanya katika nchi nyingine," Waziri Mkuu alisisitiza.

Majaliwa alisema kuwa yeye binafsi kwa kushirikiana na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, wataongoza utoaji elimu na anaamini Watanzania wataelewa malengo hayo na hasa hatua ambazo serikali inatamani kuzifikia.

**AMANI, USALAMA**

Waziri Mkuu pia alizungumzia masuala ya kudumisha amani na utulivu, mapambano dhidi ya dawa za kulevya, udhibiti wa mmomomyoko wa maadili na utunzaji wa mazingira.

Aliwataka Waislamu wanaposherehekea sikukuu hiyo, kila mmoja atambue wajibu wake wa kuwakumbuka maskini na wale wote wenye uhitaji kwa kutoa sadaka kwa maskini, ikiwa ni sehemu ya ibada za Eid el Adh'haa.

"Siku ya leo (jana) tuitumie kuwakumbuka wale ambao hawajajaliwa ili nao waweze kufurahi pamoja nasi. Tunapopata fursa ya kuchinja, tuwakumbuke waja wote wenye uhitaji, yaani yatima, wajane, wazee na makundi mengine ya watu wenye uhitaji," alisema.

Kuhusu umuhimu wa sadaka hiyo, Waziri Mkuu aliwataka watumie fursa hiyo kutafakari kwa namna gani wanampa Mungu nafasi ya kwanza katika maisha.

"Tukiona tumepwaya katika kujitoa, basi tuanze sasa kumpa Mwenyezi Mungu nafasi ya kwanza siku zote," alisema.




Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Serikali za Mtaa Wilaya ya Kinondoni, Razalous Mwakiposa (kushoto), akizungumza na wenyeviti wa kata, mitaa wa manispaa hiyo, katika mkutano uliohusu uwasilishaji wa matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2023, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia atuma salamu za Eid, asisitiza umuhimu wa amani

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewakumbusha Watanzania kuzingatia amani, umoja na upendo wakati akiwatakia kheri ya Sikukuu ya Eid el Adha.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter jana, Rais Samia aliandika; "Nawatakia nyote kheri ya Sikukuu ya Eid el Adha. Tusherehekee siku hii njema kwa amani, umoja na upendo, tukiwakumbuka wale wote wenye uhitaji zaidi.

"Tutumie siku hii pia kuendelea kumuomba Mwenyezi Mungu azipokee ibada zetu, atusamehe makosa yetu, atuongoze katika mema, kweli na haki, tuendelee kuwa wamoja na atuepushe na yote yenye nia ya kutugawa. Eid el Adh'haa Mubarak," aliandika Rais Samia.

Sikukuu hii imekuwa ikiadhimishwa baada ya Waislamu kukamilisha ibada ya Hijja ambayo ni nguzo ya tano katika nguzo za Uislamu.

Wakati huo huo, jana Rais Samia amewateua wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, Rais Samia amemteua Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Mbarouk Salim Mbarouk kuwa Makamu Mwenyekiti wa NEC kwa kipindi cha pili.

Pia, amemteua Balozi Omar Ramadhan Mapuri kuwa Mjumbe wa NEC kwa kipindi cha pili na Dk. Zakia Mohamd Abubakar, akiteuliwa kuwa mjumbe wa Tume hiyo. Uteuzi huo unaanza Julai mosi, mwaka huu. "Rais Samia amemteua Benjamin Magai kuwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Uteuzi huu umeanza tangu Juni 25, mwaka huu," ilisema taarifa hiyo.

# Mume mbaroni akituhumiwa kumwagia tindikali mke, mtoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linamshikilia Dereva wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Lusajo Mwakiwelu kwa tuhuma za kumwagia tindikali mke na mtoto huku chanzo kikitajwa wanandoa hao kuwa na mvutano wa mali baada ya kutengana.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kumfanyia tukio hilo Witness Mkivalu (31) na mtoto wake mwenye umri wa miezi minane, jana katika kituo cha stendi ya mabasi yaendayo Iringa na Mbeya cha maghorofani, jijini hapa.

Witness na mwanawe wamelazwa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma wakipata matibabu baada ya kupata majeraha ya tindikali usoni.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Martine Otieno, alithibitisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo ili kufanya uchunguzi wa tukio hilo wa kuwapo kwa mvutano kwa ajili ya kugawana mali ambazo wamechuma wote.

Alisema wanandoa hao shauri lao lilifika mahakamani kwa ajili ya kuendelea na taratibu za kisheria ambazo zilimlazimu Witness kufika Dodoma kwa ajili ya kumletea Lusajo wito wa kutakiwa kuripoti mahakamani Julai 3, mwaka huu.

"Jeshi la Polisi linaendelea na upelelezi ili kubaini zaidi kama kuna wahusika wengine ambao wamefanya kitendo hiki," alisema.

Kamanda Otieno alitoa wito kwa wanandoa wote kama inatokea wameshindwana taratibu za kisheria zifuatwe ili kuepuka kufanya vitendo vya kikatili kwa jamii hususani wanawake na watoto, ikiwamo kufanya mauaji.

Akizungumzia tukio hilo, Witness alisema amepata majeraha kwenye jicho la kushoto huku mtoto akijeruhiwa usoni.

Alisema sababu iliyomsukuma kudai talaka ni kutokana na vipigo vya mara kwa mara kutoka kwa mume wake na kuamua kuomba talaka yake na kufanikiwa kuvunja ndoa hiyo mwaka 2021.

Alisema alikwenda Dodoma kuwasilisha barua ya wito wa Lusajo Mahakama ya Wilaya ya Mufindi kwa ajili ya kusikiliza shauri lao.

Aliwashukuru madereva bajaji na pikipiki wa kituo cha maghorofani kwa msaada waliompa baada ya kutendewa tukio hilo.

# Uhaba wa dola wakwaza ununuzi, malipo tumbaku

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wengi wa tumbaku nchini hawajapata malipo yao ya minada miwili iliyopita na baadhi ya mazao yaliyovunwa yamekwama katika maghala ya vyama vya msingi vya ushirika kutokana na uhaba wa dola sokoni.

Wakulima wa zao hilo wanatakiwa kulipwa kwa dola ili kupunguza kupungua kwa thamani ya zao hilo katika fedha za kigeni kwa wakulima, kutokana na aina ya mnyororo wa thamani wa mazao, kama ilivyoelekezwa na serikali.

Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Victor Mwambalaswa, alimwambia mwandishi jana kuwa uhaba wa dola ni tatizo la dunia, lakini wanalifanyia kazi suala hilo ili kuhakikisha changamoto hizo zinatatuliwa na wakulima wanalipwa.

"Unajua shida ya upatikanaji wa dola sasa ni suala la kimataifa, lakini tunalifanyia kazi," alisema jana katika mazungumzo na mwandishi aliyetaka kujua kiini cha tatizo na hatua zinazochuliwa.

Alisema wakulima wa tumbaku wanalipwa kwa dola kwa sababu walipata pembejeo kwa utaratibu wa kimkataba na wanunuzi kwa thamani ya fedha za kigeni na hii inafanyika ili kuepusha upotevu wa thamani ya fedha.

Mwenyekiti wa Bodi alisema tayari wameziarifu benki za biashara, ambazo zilitoa mikopo ya pembejeo kwa wakulima kuhusu kero hiyo.

"Mnunuzi mmoja wa tumbaku alilalamikia ukosefu wa fedha za kununua tumbaku na benki ilitoa utaratibu wa kufadhili kuhakikisha kuwa mkulima analipwa," alisema.

Jana, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Masoko ya Kilimo cha Matabalo (AMCOS) kilichoko wilayani Kasulu mkoani Kigoma, Gabriel Ntalagana, alisema wanachama wake wengi hawajalipwa fedha za minada miwili iliyopita.

"Tumeripoti hili kwa chama cha ushirika cha mkoa na Msajili wa Vyama vya Ushirika," alisema.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, wakulima wanatakiwa kulipwa ndani ya siku 14 baada ya ununuzi wa zao hilo, akirejea makubaliano ya kilimo cha kimkataba, lakini tayari zimepita siku 21 tangu kununuliwa kwa zao hilo kupitia mnada wa pili uliokuwa na jumla ya dola za Marekani 288,000.

Lakini kiongozi huyo alikiri kuwa katika mnada wa kwanza, wanunuzi walifanya malipo wiki moja baada ya ununuzi wa zao hilo.

Alisema waliomba iwapo kutakuwa na uhaba wa dola, fedha za ndani zitumike kuwalipa wakulima kwa kuzingatia kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni, kwa kuwa mikopo ya pembejeo tayari imelipwa kwa fedha za kigeni.

"Tulifanya mnada wetu wa tatu hivi karibuni na bado tunakusanya takwimu ili kujua mapato ya jumla ya kulipwa kwa wakulima," alisema.

Mwenyekiti wa AMCOS ya Lupa ya mkoani Rukwa , Msingija Jilala, pia alisema wanakabiliwa na changamoto ya malipo kwa wanachama wake kwa kuwa kampuni za kununua nazo zinalalamikia uhaba wa dola.

Hata hivyo, alisema wamepata angalau sehemu ya malipo hayo siku mbili zilizopita, japo walifikia hatua ya kugomea utoaji wa zao hilo katika maghala na wanunuzi.

"Kuna baadhi ya vyama vyetu vya msingi vya ushirika ambavyo vimesusia ununuzi wa mazao hadi malipo yao ya mnada wa awali yatakapokamilika," alisema.

Aliitaka serikali kuongeza muda wa ununuzi wa tumbaku uliowekwa kufikia leo hadi angalau mwezi mmoja ujao kutokana na changamoto ya usafirishaji wa tumbaku zinazojumuisha ubovu wa miundombinu ya barabara.

HABARI KITAIFA

# ACT kuteua wagombea wanawake uchaguzi ujao

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ado Shaibu, amesema chama hicho kimejipanga kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi.

Amesema mkakati huo utatiliwa mkazo katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani na Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Mtendaji huyo wa chama aliyasema hayo katika mikutano mikuu ya baadhi ya majimbo ya mkoani Tanga iliyofanyika kwa siku tofauti kuanzia Juni 26 mwaka huu huko Pangani na Mkinga.

"Nimefarijika na ushiriki mkubwa wa viongozi wanawake katika kata, wao ndiyo wajumbe wa Mkutano Mkuu. Hali hii inatia moyo kwa sababu ukombozi wa kweli wa jamii yetu kisiasa, kiuchumi na kijamii utapatikana iwapo wanawake watashiriki ipasavyo.

"Hatupaswi kuishia katika ngazi ya kata pekee. Ni lazima wanawake wajitokeze kwa wingi zaidi kugombea ngazi za jimbo, mkoa na Taifa. "Wanawake pia jipangeni kushiriki kwa wingi katika uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu kwa nafasi mbalimbali," alihamasisha.

Pia alisema chama kimejipanga kuwajengea uwezo wa kiongozi viongozi wanawake katika ngazi za majimbo ili washiriki ipasavyo katika uchaguzi ujao.

Juzi, Katibu Mkuu huyo alihitimisha ziara yake ya siku tatu mkoani Tanga. Katika ziara hiyo, Ado alitembelea majimbo ya Tanga Mjini, Pangani na Mkinga na kukutana na viongozi wa kata 63 za majimbo hayo kupitia mikutano mikuu ya majimbo.



Baadhi ya wafanyakazi wa Taasisi ya Ishik Medical Foundation na wakishirikiana na Feza School, wakichinja ng'ombe kwa ajili ya kugawa sadaka kwa waumini wa Kiislam na watu wasiojiweza pamoja na watoto yatima, jijini Dar es Salaam jana, kwa lengo kusherehekea Sikukuu ya Eid al Adha kwa pamoja na wananchi wote. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Migogoro ya ardhi Dodoma yashtua, mkakati wasukwa

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesema wizara yake imeweka vipaumbele 12 katika mwaka ujao wa fedha 2023/24 unaoanza kesho, lengo kubwa likiwa kuondoa changamoto za sekta ya ardhi na kutilia mkazo ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, katika kipindi cha mwaka huo wa fedha, Wizara ya Ardhi imejipanga kuhakikisha mikakati yake inakwenda vizuri hususan kuondoa kero na malalamiko ya wananchi kwa kuwa dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha nchi inakuwa kiuchumi na watu wake wanafaidika na mali waliyokuwa nayo ambayo ni ardhi.

Dk. Mabula alisema hayo juzi muda mfupi baada ya kikao cha uongozi wa wizara kwa ajili ya kuweka mikakati ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara ya Ardhi baada ya kumalizika kwa Bunge la Bajeti 2023/24.

Alisema kuwa kabla ya viongozi kuanza kuzuru maeneo mbalimbali, ameona wakutane na kuweka mikakati ya namna bora ya kufanyia kazi wanayotarajia kuyafanya katika mwaka wa fedha ujao.

"Kama wizara tumejipanga na tunatembelea maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambaye amaeonyesha njia na tunafuata nyayo zake kuhakikisha changamoto, dhulma, migogoro, malalamiko hayana nafasi katika kipindi hiki na tutahakikisha watendaji wa sekta ya ardhi wanajipanga sawasawa katika kutenda kazi hiyo," alisema.

Katika kutekeleza viaumbele hivyo, Waziri Mabula alisema moja ya mambo wanayokwenda kuyawekea mkazo ni suala la migogoro ya ardhi ambapo wizara yake kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji inakwenda kuweka mikakati ya kumaliza migogoro, ukiulenga zaidi Mkoa wa Dodoma.

"Mkoa wa Dodoma tumeulenga zaidi kutokana na kukithiri kwa migogoro ya ardhi ambapo kama wizara tumeona mkoa huu sasa uwe na Kamishna wa Ardhi Wasaidizi wawili, mmoja atashughulika na jiji huku mwingine akishughulika na wilaya zilizopo pembezoni," alifafanua.

Akielezea zaidi vipaumbele hivyo, Dk. Mabula alisema suala la makusanyo ardhi litatiliwa mkazo, ikizingatiwa Rais Samia ameshusha gharama za umilikishaji ardhi na wizara yake inakwenda kuwatangazia wananchi ushushwaji wa gharama hizo.

Sera na sheria za ardhi ni jambo lingine linalopewa kipaumbele, ikizingatiwa tayari serikali imeleta nafuu wa gharama katika uhamisho wa milki kutoka asilimia 10 hadi tatu sambamba kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa ununuzi wa nyumba za gharama nafuu.

Kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi, Dk. Mabula aliweka wazi kuwa vijiji vingi vimepimwa na kati ya12,000, vijiji 10,000 vimepimwa na vina vyeti lakini changomoto ni mipango ya matumizi ya ardhi kutovifikia baadhi ya vijiji na kusisitiza kuwa, mamlaka za upangaji ambazo ni halmashauri zinatakiwa kuongeza kasi katika suala hilo kwa kushirikiana na tume.

Waziri Mabula pia alizungumzia Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumikilisha Ardhi (KKK), akisema changamoto kubwa ya mradi huo ni kutorejeshwa mikopo kwa wakati na kueleza kuwa wizara yake inaangalia namna ya kuhakikisha fedha zinarejeshwa kwa wakati.

Vilevile, alisema wanatilia mkazo matumizi ya Tehama katika utendaji wao, pia uendelezaji milki ambao Dk. Mabula aliutaja ni sekta ambayo haijaendelezwa kwa kiasi kikubwa, hivyo wizara yake itatupia jicho zaidi eneo hilo pamoja na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia mpya.

Vipaumbele vingine kwa mujibu wa waziri huyo ni pamoja na utoaji elimu kwa umma, masuala ya uwekezaji, uimarishaji mipaka ya kimataifa na fursa ya wananchi kutumia Kituo cha Mawasiliano kwa Wateja kitakachowawezesha kupatiwa huduma bila kufika ofisi za ardhi.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**PASCAL AKO MALACK** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **LANDROVER 110** yenye usajili namba **T536 DJH, CHASSIS NAMBA: SALLDM71497495** na **ENGINE NAMBA: 16130296A.** kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/220293/2023**


# TNBC yasifu Rais Samia mazingira bora biashara

**Na Mary Geofrey**

BARAZA la Taifa la Biashara (TNBC), limesema mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji yameboreshwa sambamba na kuvutia uwekezaji nchini chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mafanikio ambayo baraza limeyapata.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu mambo makubwa yamefanyika ikiwamo maboresho ya sera, kuondoa tozo mbalimbali na kutokomeza ukiritimba uliokuwa unakwamisha ustawi wa biashara na uwekezaji nchini.

"Katika kipindi cha miaka mitatu, Rais Samia ameifungua nchi kiuchumi ikiwamo kuimarika kwa ushirikiano na uhusiano kati ya sekta binafsi na umma na utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara (MKUMBI) ili kuvutia uwekezaji na kukuza biashara nchini," alisema Dk. Wanga.

Alibainisha kuwa chini ya Uenyekiti wa Rais Samia, baraza limefikia malengo yake ikiwamo kuimarika kwa mabaraza ya biashara ya mikoa (RBC) na mabaraza ya biashara ya wilaya (DBC) kama sehemu ya kupata mrejesho, pia kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara kupitia mikutano yao ya majadiliano.

"Lengo la kuanzisha mabaraza hayo katika ngazi ya mikoa na wilaya ni kuwezesha serikali za mitaa kushughulikia changamoto za biashara na uwekezaji katika halmashauri pale ambapo kuna mwingiliano wa mara kwa mara na wafanyabiashara," alisema.

Dk. Wanga alisema chini ya uongozi wa Rais Samia, serikali imeondoa tozo na makato mbalimbali na hivyo kupungua kwa gharama za kufanya biashara nchini sambamba na kuongeza thamani katika bidhaa zinazozalishwa na huduma.

"Hii miaka mitatu ya uongozi thabiti wa Rais Samia, tumepiga hatua kubwa katika kuvutia uwekezaji nchini kwani tumekuwa tunafanya maboresho mbalimbali ikiwamo kuondoa tozo na makato na hivyo kuwezesha kampuni kujitengenezea faida na kukuza mitaji yao," alisema Dk. Wanga.

## TANGAZO

The Guardian
www.ippmedia.com
The Home of Great Newspaper

# Our Regional Offices and Representatives




*Feel free to contact for:*

**ADVERTISEMENT ON NEWSPAPERS / DIGITAL PLATFORMS AND SUBSCRIBING NEWSPAPERS / E-PAPERS**

**HEAD OFFICE**

THE GUARDIAN LIMITED
MIKOCHENI AREA
P.o.Box 31042, Dar es salaam, Tanzania
Tel: + 255 745700710 | Email: info@guardian.co.tz

Nipashe @Nipashetz
The Guardian @Theguardiantz
IPPmedia.com

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mawaidha ya viongozi wa dini yawe mafunzo kwa waumini

**JANA** Waislam kote nchini walisherehekea Sikukuu ya Eid Mubarak ikiwa ni siku ya kumbukumbu ambayo waumini wa dini ya Kiislamu walikamilisha nguzo ya tano ya Uislam ambayo ni Hijja.

Kipindi hiki ndicho Waislam hukitumia kwenda kuhiji wakiungana na wenzao wa mataifa mengine duniani.

Wakati akizungumza na waumini hao, Kaimu Mufti, Shekhe Ally Khamis Ngeruko amewakumbusha viongozi wa dini hiyo kuweka mipango ya kuwainua kiuchumi Waislamu nchini ili wanapokwenda kuhiji watafute pia fursa za kiuchumi.

Amewataka Waislamu kufunua akili zao katika kupambana na kujiingiza kwenye miundombinu ya kiuchumi ambayo serikali imewaandalia huku akiwakumbusha kuwa Hijja ni fursa na kwamba mji wa Makka kuna soko la kimataifa, akiwahimiza wamachinga wa kimataifa waende kupeleka bidhaa za kitanzania.

Jambo la msingi alilolikumbusha Mufti Khamisi ni jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akihangaika usiku na mchana kutafuta wawekezaji ili kunyanyua uchumi wa Tanzania. Juhudi hizo za Rais Samia, zimeanza kuzaa matunda baada ya wawekezaji kutoka nchi mbambali duniani kuingia nchini kutafuta fursa.

Pia, katika salamu za Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), limezungumzia umuhimu wa sikukuu hiyo kwa kuwa inakumbusha siku ambayo waumini wenzao walikamilisha nguzo ya tano ya Uislamu ambayo ni Hijja.

BAKWATA imeahidi kuendelea kuwaunganisha Waislamu nchini na kukemea tatizo la mmomonyoko wa maadili ambalo limeikumba Tanzania na limehimiza malezi mema kutoka kwa wazazi na walezi. Limewaasa Watanzania kuhusu Tanzania kukumbwa na wimbi la mmomonyoko wa maadili unaopandikizwa na tamaduni za kigeni likiwamo suala la ushoga. "BAKWATA tunaendelea kulaani sana na kukemea vitendo hivyo na tunaendelea kusisitiza kuhusu malezi mema ya vijana wetu ili kuwakuza katika maadili mema."

Baraza hilo limezungumzia umuhimu wa wazazi kusimamia misingi imara katika familia zao ambako ni chimbuko la tabia njema linalotokana na malezi ya familia. Uislamu umehimiza tabia njema na

umezingatia imani ya mtu kutokana na mema yake. "Tukiyatekeleza haya kwa vitendo, tunaamini tutakuwa na kizazi chema ili kujenga Taifa lililo imara na la watu waadilifu, wasio wala rushwa, wasio mafisadi na wenye kujali haki za wenzao."


Mawaidha mazuri yaliyotolewa na viongozi wa dini ni lazima yazingatiwe kwa kuwa matamshi yao ni agizo linalotoka kwa Mungu kupitia wao.

Viongozi wa dini wana nguvu kubwa katika ushawishi wa kubadili tabia za watu na vilevile wanaaminiwa kutokana na karma waliyonayo.

Ndiyo maana hata viongozi wa kiserikali wanapokwama katika jambo fulani, huwafuata viongozi wa dini wasaidie kutoa mwongozo na pia kutuliza mazingira yanayoonekana kuchafuliwa na uzushi na upotoshaji.

Sikukuu za kidini husaidia kuwakutanisha waumini wake na kuongea lugha moja, hivyo ni muhimu sana viongozi wa dini wanapotoa ushauri, mwongozo ufuatwe ili watu waendelee kufarahia amani waliyo nayo na pia kuishi kwa upendo bila kuwa na chuki. Tanzania imebarikiwa kwa kuwa wananchi wake wote wanaongea lugha moja hivyo ni rahisi watu kusikilizana na kuelewana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Tujipe wajibu, tushirikiane kudhibiti hizo dawa za kulevya kona zake zote

Na Sabato Kasika

**MAMLAKA** ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA), imeepusha watu milioni tano katika matumizi ya dawa za kulevya, pia kukamata watuhumiwa 109 wakiwa na dawa hizo.

Baadhi ya dawa zinazotajwa kunaswa na mamlaka hiyo ni heroin, cocaine, bhangi kavu, mbichi, iliyosindikwa na pia kuteketeza ekari 1,093 za mashamba ya dawa hizo sehemu mbalimbali nchini.

Kwa mujibu wa Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, kiasi cha heroin kilichokamatwa kati ya Machi 25, 2023 hadi Juni 19, 2023 iwapo kingeingia sokoni, kingeweza kutumiwa na kuathiri watu milioni 4.815.

Ninadhani kwa maelezo hayo, ni wazi ipo haja kwa Watanzania kuwapa ushirikiano DCEA katika vita hii ili waweze kuifanikisha, hasa kutokana na ukweli kwamba dawa hizo zinaathiri taifa la kesho.

Pia, sidhani kama kuna Mtanzania anayeunga mkono biashara hiyo haramu iendelee. Hivyo ni vyema, tutoe ushirikiano kwa mamlaka husika kwa kutambua kuwa vita hiyo inahushisha jamii nzima.

Katika maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani yaliyofanyika jijini Arusha hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan alisema Tanzania imefanikiwa kuzuia uingizaji wa dawa za kulevya kwa asilimia 90 ambapo hivi sasa dawa za kienyeji kama bhangi zimekuwa kinara katika tatizo kubwa.

Wakati nchi ikiwa imefanikiwa kwa asilimia hiyo, ninadhani sasa ni vyema kushirikiana na mamlaka hiyo ya serikali ili asilimia 10 iliyobaki iishe na kuwa na asilimia sifuri ya matumizi ya dawa hizo. Pia watumishi wa umma kuweka uzalendo mbele ili kusimamia maslahi ya taifa kwa kutojihusisha kwa namna yoyote na biashara ya dawa hizo, ili kuokoa kizazi kijacho.

Ninasema hayo, kwa kuwa hata Rais mwenyewe alitoa rai kwa jeshi la polisi kutowabambikiza wananchi kesi kwa sababu ya chuki bali watende haki ili kuepuka chuki kwa wananchi.

Wazazi na walezi nao hawana budi kusimamia vyema majukumu yao, huku viongozi na jamii nayo ikishirikiana na viongozi wa mila ili kusaidia kusimamia maadili mema.

Aidha, Rais ameshafafanua kuwa, serikali imetenga fedha Sh. bilioni 24 .41 kwa ajili ya kuwezesha kupambana na hatimaye kumaliza balaa hilo linalotokana na matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Ninadhani tungezionea huruma fedha hizo, kwa kushirikiana na serikali katika vita hii, kwa kutoa taarifa ni wapi zinakouzwa au zinaingizwaje, ili kusaidia kudhibiti uingizwaji na matumizi yake.

Hayo yakifanyika, yawezekana tukaokoa fedha hizo zikaenda kwenye shughuli nyingine za maendeleo ya nchi. Bila jamii kushiriki kwa kutoa taarifa, ni wazi matumizi yataendelea kuwepo na hivyo kusababisha serikali kuendelea kutumia gharama kubwa kuwahudumia waathirika.

Ikumbukwe kuwa utafiti uliofanywa na (TMDA) maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), umebaini uwepo wa baadhi ya watumiaji wa shisha.

Kwa mujibu wa utafiti huo ni kwamba, watumiaji wa shisha huchanganya dawa za kulevya aina ya heroine na cocaine na kuchangia kuwapo kwa ongezeko la biashara za dawa za kulevya.

Utafiti huo nao unaonyesha jinsi gani jamii bado ina nafasi ya kushiriki katika vita ya dawa za kulevya katika maeneo mbalimbali nchini ili kuokoa vijana wa Kitanzania.

Ikumbukwe kuwa DCEA imeshafafanua kuwa vijana wanaojihusisha na matumizi ya dawa hizo ni wa umri wa kuanzia miaka 11, ambao kimsingi ni taifa la baadaye.

# Mvinyo wa Tanzania kupata soko China

**Na Mwandishi Maalum**

KWENYE shamba la mizabibu lenye ukubwa wa hekta 1.5 umbali wa takribani kilomita 39 Kaskazini mwa Mji Mkuu wa Tanzania, Dodoma, William Swai, anakagua zabibu chini ya jua kali.

Hadi kufika katikati ya mwezi Julai, zabibu zitakuwa zimeiva na zitachumwa kutengeneza mvinyo wenye ladha nzuri, mkulima huyo wa zabibu mwenye umri wa miaka 67 ameliambia Shirika la Habari la China, Xinhua katika mahojiano.

"Kufunguliwa kwa masoko ya kimataifa, likiwamo la China, kwa mvinyo unaotengenezwa nchini kutaongeza uzalishaji wa viwanda vya mvinyo nchini," alisema.

Licha ya Tanzania kutokuwa na sifa ya kimataifa ya kuwa mzalishaji wa mvinyo, ni nyumbani kwa eneo la pili kwa ukubwa kwa uzalishaji wa kinywaji hicho kwenye eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara baada ya Afrika Kusini.

Aina za zabibu zinazojulikana mkoani humo ambako tasnia ya mvinyo ya Tanzania imejikita zaidi, ni Chenin Blanc, Syrah, Cabernet Sauvignon, na aina nyingine iliyopewa jina la eneo moja la Dodoma, Makutupora.

Hapo awali, ulimaji wa zabibu na uzalishaji wa mvinyo ulikuwa ukifanywa na wamisionari pekee, lakini kuanzia mwaka 1969 Serikali ya Tanzania iliingia kwenye soko la biashara hii kwa kuunda Kampuni ya Mvinyo ya Dodoma.


Archard Kato, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Alko Vintages, kampuni ya Tanzania inayotengeneza chapa kadhaa za mvinyo, ameliambia Xinhua kuwa kampuni yake hailimi zabibu, bali inapata kutoka kwa vikundi 15 vilivyoandaliwa vya kilimo cha zao hilo ambavyo vinaipatia kampuni hiyo zabibu zenye sifa bora.

"Tunasimamia uzalishaji wao. Tunalipa wataalam kutoka Afrika Kusini na Italia kuwasaidia wakulima kuzalisha zabibu bora na usimamizi mzuri wa mizabibu," alisema.

Miaka minne iliyopita, kampuni hiyo ya Tanzania ilianza kufanya kazi na Kampuni ya Usambazaji ya Weihai Huatan ya China kusafirisha mvinyo nchini China. Kampuni hiyo ya China inajishughulisha zaidi na biashara ya kimataifa, maendeleo ya kilimo, ujenzi wa miradi nje ya nchi, uwekezaji wa viwanda, na shughuli nyingine.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Wang Xiangyu, alisema kampuni hiyo ilianza kuagiza mvinyo wa Tanzania mwaka 2018 na kuwa wakala mwenye haki za kipekee wa mvinyo wa Tanzania, huku ikiagiza chupa zaidi ya 30,000 za mvinyo.

Wang alisema kwa kutambulisha mvinyo wa Tanzania katika soko la China, wanunuzi wa nchi hiyoa watakuwa na chaguo pana na kubwa zaidi la aina za mvinyo na kuruhusu bidhaa kutoka Afrika kuonekana kwenye meza za wanunuzi wengi zaidi wa China.



Archard Kato, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Alko Vintages, akizungumza kwenye mahojiano na Shirika la Habari la China, Xinhua ofisini kwake mjini Dodoma. **PICHA: HERMAN EMMANUEL/XINHUA**

# Wakazi 20,000 Kata Kitopeni kuondokana shida ya maji

**Na Joseph Mwendapole**

UTEKELEZAJI wa mradi wa maji Kitopeni, Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam umefikia asilimia 98 na unatarajiwa kuwanufaisha wananchi 20,000.

Ujenzi wa tangi la ujazo wa lita 90,000 umekamilika kwa asilimia 100.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, msimamizi wa mradi kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Mhandisi Aziz Namanga, alisema utaanza kuwanufaisha wananchi hao hivi karibuni.

"Kazi ya utekelezaji wa mradi huu imefika asilimia 98, na kwa sasa tumefanikiwa kumaliza ujenzi wa tangi la ujazo wa lita 90,000 na kazi iliyobaki na ulazaji wa mabomba ya kusambazaji maji," alisema Mhandisi Namanga.

Alisema kazi nyingine inayoendelea kutelekezwa kwenye mradi huo ni ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji ya inchi tofauti tofauti kama vile inchi 8, 6, 4, 2, 1.5 kwenda kwa wananchi.

"Kukamilika kwa kazi ya mtandao wa mabomba inayotekelezwa kutatoa fursa ya namna ya kuwahudumia wananchi kupitia mradi huu," alisema Mhandisi Namanga.

Pia, utekelezaji wa mradi umefika hatua nzuri na wana matumaini ya kukamilika kwa mradi huo mwezi Julai, mwaka huu kwa kuwa kazi inafanyika usiku na mchana ili kuhakikisha unakamilika ndani ya wakati.

Meneja wa Mkoa wa Huduma DAWASA, Ubungo Mhandisi, Edson Robert, aliwataka wananchi wajiandae kupokea mradi kwa kuwa unaenda kuondoa shida ya maji.

Naye, Mwenyekiti wa Mtaa wa Makabe, Peter Lushiku, aliishukuru serikali kupitia DAWASA kwa jitihada za kuwaondoa wakazi wa Mbezi Makabe kwenye shida ya maji na kusisitiza wananchi kuendelea kuwa watulivu wakati mradi unaelekea kukamilika.

"Tunaishukuru DAWASA kwa kutusaidia kutuleta huu mradi ambao utatusaidia kutupatia huduma ya maji ambayo tulikuwa tunaikosa kwa muda mrefu," alisema Lushiku.

Kukamilika kwa mradi huo ambao unatekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani Sh. milioni 740.6 ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023 kutanufaisha wakazi wa maeneo mbalimbali kupata huduma, Makabe, Msakuzi kaskazini, Makabe mpakani na mradi unatekelezwa na kampuni ya mkandarasi ya SAMKA.

**KABWELA** — **Na Fadhili Mohammed**





Mtaalamu Mwandamizi wa Fedha kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa (UNCDF) na Meneja wa Programu ya CookFund, Immanuel Muro (kulia), akifafanua jambo kuhusu programu hiyo yenye udhamini wa Euro milioni 17 kutoka Umoja wa Ulaya (EU) kwa wakuu wa programu wa umoja huo, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Wengine ni Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Manfredo Fanti (wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa Idara ya Nishati wa EU, Massimiliano Pedretti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Othman azikumbusha taasisi utatuzi changamoto kijamii

**Na Frank Monyo**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, amezitaka taasisi zinazojishughulisha na masuala ya uhisani Afrika Mashariki, kuongeza nguvu kutatua changamoto zinazoikabili jamii ili kuimarisha ustawi wa wananchi.

Wito huo aliutoa jana, visiwani Zanzibar wakati akifungua mkutano wa nane wa Uhisani Afrika Mashariki (EAPC), ulioandaliwa na Mtandao wa Uhisani Afrika Mashariki (EAPN), kwa kushirikiana na Taasisi ya Legal Services Facility (LSF).

Alihimiza kuimarishwa kwa umoja na nguvu kwa taasisi hizo katika kukabiliana na changamoto zinazohitaji juhudi za pamoja kuzitatua, ikiwemo mabadiliko ya hali ya hewa, umasikini, ukosefu wa usawa na athari zilizotokana na janga la ugonjwa wa virusi vya Corona (UVIKO-19).

"Mabadiliko ya mifumo yenye athari yanahitaji mbinu ya kina na jumuishi ambao inavuka mipaka ya jiografia, itikadi na sekta.

Ni kupitia ushirikiano thabiti wa ndani, kikanda na kimataifa ndipo tunaweza kutumia nguvu kubwa ya hatua za pamoja ili kukabiliana na changamotoi nyingi mbele yetu," alisema Othman.

Alisema kaulimbiu ya mkutano huo ya "Mabadiliko ya mifumo: kuchochea hatua za pamoja" inaunga mkono dhamira ya Zanzibar katika kukabiliana na changamoto za kimfumo.

"Tunabaki katika harakati zetu za kufungua uwezo uliofichika ndani ya mifumo yetu ili kuunda jamii ambayo siyo tu yenye ustawi na endelevu, bali pia jumuishi kwa uthabiti."

Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema nguvu ya taasisi za uhisani Afrika, imeelekezwa katika kuwezesha jumuiya zenye maendeleo endelevu, ambapo zimekuwa zikitoa rasilimali, utaalamu na mitandao ili kukuza mabadiliko ya kudumu.

Lulu, alisema mkutano huo wa siku tatu, ulioanza jana Juni 28 hadi 30 Juni 2023, unalenga kuangalia namna ya kuongeza juhudi za ushirikiano wa taasisi za uhisani ili kukuza mazingira yanayofaa kwa ukuaji wa uhisani barani Afrika.

"Sisi LSF, tunapenda kusikia mitazamo yote na tunaamini kwa uthabiti majadiliano katika jukwaa hili, yanaweza kuwa hatua nyingine muhimu kuelekea mabadiliko ya mifumo kote na kwa hivyo, kuongoza juhudi za maendeleo endelevu. Nawatakia mapumziko mema Zanzibar," alisema Lulu.

# Mbunge ahoji wakulima wa kahawa kutolipwa fedha zao

**Na Mwandishi Wetu,**

DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, ameviagiza vyama vya ushirika, ambavyo havijawalipa wakulima wa kahawa tangu mwaka jana, viwalipe fedha zao mara moja ili waendelee na msimu mpya wa kilimo.

Mavunde alitoa agizo hilo juzi bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Vwawa, Japhet Hasunga (CCM), aliyehoji lini wakulima hao watalipwa fedha zao na vyama vya ushirika.

Mavunde, akijibu swali hilo, alisema "...biashara ya mazao ni kama zilivyo biashara nyingine. Ninatumia nafasi hii kuwataka wote ambao hawajawalipa wakulima, wawalipe mara moja kabla ya msimu mpya wa kilimo."

Kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, mauzo ya kahawa nje ya nchi kwa mwaka 2021/22, yalikuwa tani 66,543 zilizoiingizia nchi dola za Marekani 204,194,355.

Waziri huyo alibainisha kuwa hadi kufikia Aprili mwaka huu, kahawa iliyokuwa imeuzwa nje kwa mwaka huu wa fedha (2022/23) ni tani 71,120, nchi ikipata dola za Marekani 204,670,145.

Vilevile, kwa mwaka huo ambao Mbunge Hasunga analalamika wakulima hawajalipwa fedha zao, kulikuwa na mikopo ya Sh. bilioni 57.486 iliyotolewa kwa vyama vya ushirika vitano na kampuni mbili kwa ajili ya ununuzi wa kahawa katika Mikoa ya Kagera, Mara na Mbeya kwa msimu wa mwaka 2022/23.

# Jafo: Bajeti imezingatia uhifadhi wa mazingira

**Na Robert Hokororo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amesema bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24 imezingatia uhifadhi wa mazingira.

Aliyasema hayo juzi mara baada ya kuahirishwa kwa Mkutano wa 11 wa Bunge wakati akitoa tathmini kuhusu hotuba ya bajeti hiyo iliyowasilishwa na serikali hivi karibuni.

Dk. Jafo alisema bajeti imegusa wizara za kisekta kwa upande wa mazingira kwa kuwa zimetengewa bajeti inayotosha kutekeleza miradi ya mazingira.

Alisema bajeti imetenda haki kwa upande wa mazingira kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ndiyo inayoratibu sekta hiyo, imetengewa fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uhifadhi wa mazingira.

Waziri Jafo alisema ana imani kwamba katika bajeti ya mwaka huu kwa kiwango kikubwa Tanzania imetoa mchango mkubwa duniani katika suala la kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Akitolea mfano, Dk. Jafo alisema Wizara ya Kilimo imetengewa bajeti kubwa kwa ajili ya utengenezaji wa mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji hususan katika maeneo yaliyoathirika na changamoto hiyo.

Waziri Jafo pia alisema kuwa bajeti imeinufaisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo imetengewa fedha kwa ajili ya uchimbaji wa malambo ya kunyweshea mifugo hasa katika maeneo kame.

Alisema miradi ya kimkakati ikiwamo bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere pamoja na nishati jadidifu imetengewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake ambayo itasaidia kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

Kwa mujibu wa Waziri Jafo, Reli ya Kisasa (SGR) inayoendelea kujengwa itatumia nishati ya umeme badala ya mafuta, hivyo kupunguza uchafuzi wa mazingira unaotokana na moshi.

Hivi karibuni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwasilisha bajeti ya Sh. trilioni 44.38 ambayo tayari imepitishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji.



# Tume ya TEHAMA yajivunia ukuzaji teknolojia

**Na Godfrey Mushi,**
ARUSHA

TUME ya TEHAMA nchini (ICTC), imepata mafanikio makubwa katika ukuzaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano, kusajili taasisi ndogo za TEHAMA na kutoa miongozo.

Mkurugenzi Mkuu wa tume hiyo, Dk. Nkundwe Mwasaga, aliyasema hayo jana jijini Arusha, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo makamishna wa tume hiyo. Alisema wameamua kutoa mafunzo maalumu na kujadiliana ni namna gani nchi nyingine duniani zinafanya ili kuongoza taasisi zao na wanatumia nyenzo gani kuendesha taasisi zao.

"Tume ina majukumu makuu mawili, kwanza ni kuratibu utekelezaji wa Sera ya TEHAMA ya Taifa na jukumu la pili ni kukuza TEHAMA.

"Hivyo, tumekuja kwa ajili ya mafunzo mbalimbali Arusha na tuna wawezeshaji kutoka Taasisi ya Uongozi na Ofisi ya Hazina nchini. Kimsingi, tunatarajia kupata uelewa wa kutosha kuhusu mipaka ya makamishna wa tume, uongozi wa taasisi."

Mkufunzi wa mafunzo hayo kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Prof. George Oreku, alishauri serikali iweke msukumo mkubwa kwenye ICT, hususani kwa vijana kutokana na teknolojia kuwa kubwa na huko tuendako mambo yatabadilika zaidi.

"Ni vyema vijana wengi wakapikwa na Tume ya TEHAMA kwa sababu masuala ya ulinzi wa kimtandao ni makosa ya kimtandao vyote hivi vinafanyika mitandaoni."

Prof. Oreku, aliishauri serikali kuanzia sasa kuona umuhimu wa kufanya uteuzi wa wajumbe wa bodi kulingana na maeneo sahihi ili aliyeteuliwa awe na wigo mpana kulingana na utekelezaji wa majukumu katika taasisi husika.

"Watendaji wa bodi wapewe mafunzo ya kutambua mipaka yao ili kuleta ufanisi katika majukumu yao bila kuvuka mipaka ya kazi,"alisisitiza Prof. Oreku.

Naye Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Dk. Faisal Issa, alisema mafunzo hayo yatawajenga kwa kuwapa upeo wa kutenda vyema katika majukumu yao.

Alisema: "Tume hii imeanza hivi karibuni na hii ni bodi yake ya kwanza. Kwa hiyo yapo masuala machache ya kiutendaji ambayo yanahitaji muda; na michakato inaendelea na nyaraka zikikamilika itatenda kazi kwa ufanisi zaidi".



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini, Dk. Nkundwe Mwasaga (aliyenyoosha mkono), akizungumza na wadau mbalimbali, wakati wa mafunzo ya masuala ya Tehama, jijini Arusha juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wananchi wawatuhumu viongozi kuchochea mgogoro

**Na Allan Isack,**
SIMANJIRO

MGOGORO mpya unaohusu uanzishaji mnada wa mifugo na soko jirani na kata mbili zinazopakana katika Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara na Arumeru mkoani Arusha, unafukuta baada ya wananchi kuanza kuwatuhumu viongozi kutengeneza vita ya kiuchumi na uhasama.

Kwa nyakati tofauti jana, wakazi wa Kijiji cha Shambarai, Wilaya ya Simanjiro waliwashutumu viongozi wa Kata ya Shambarai Burka, Wilaya ya Arumeru, kuanzisha mnada na soko jirani nao, jambo ambalo limesababisha mnada wao kufa.

Kutokana na hali hiyo kujitokeza, Mkazi wa Shambarai (Simanjiro), Eliaman Stephano, aliiomba serikali kuingilia kati suala hilo, kwa kuwa litatengeneza uadui na wananchi wanaweza kudhuriana kwa chuki zinazojengwa na viongozi wanaotengeneza maslahi yao ya kisiasa.

"Huu mnada ulianzishwa miaka ya 70 na Shambarai Burka wakaanzisha miaka ya 1990. Lakini kinachoendelea baada ya upande wetu soko na mnada kufa linaweza kuleta shida," alisema.

Mkazi wa kijiji hicho, Eliaman Stephano, alisema wananchi wa eneo hilo wana nyaraka za uanzishwaji soko na mnada lakini majirani zao hawana vibali.

"Mnada wetu ulikuwepo tangu miaka ya zamani wakati Rais wa Tanzania akiwa Julius Nyerere, haiwezekani watu wengine waanzishe mnada jirani na sisi na kuua soko na mnada wetu wa miaka mingi serikali iingilie kati jambao hili," alisema.

Naye Japhet Daniel, alisema baadhi ya wananchi wa eneo hilo, wamechukua mikopo kwenye taasisi za kifedha ila wanashindwa kurejesha baada ya mnada huo kufa.

"Watu wamechukua mkopo kufanya biashara, hii ni hujuma inafanyika kwani huwezi kutoka hapa uende jirani na Kijiji cha Naberera ukaanzisha soko pale hivyo hatua zichukuliwe ili kunusuru soko hili la Shambarai,"alisema Daniel.

Alipotafutwa kuzungumzia mgogoro huo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Shambarai, Merinyo Mollel, alisema wizara husika inapaswa kuingilia tatizo hilo, kwa kuwa sheria za minada na masoko inaagiza kuanzisha mnada mwingine umbali wa kilomita saba na ulioko ni kilomita nne tu.

Naye, Diwani wa Kata ya Shambarai Burka, John Mollel, alisema ni wakati muafaka kwa wananchi wa Shambarai kuboresha soko lao na mnada ili wateja waamue wenyewe sehemu ya kwenda.

"Huu ni mgogoro wa muda mrefu, tangu hii kata ilipomegwa Mbuguni na Diwani akiwa marehemu Thomas Mollel (askofu) na ilikutanisha viongozi waliokuwa wakuu wa mikoa, Henry Shekifu (Manyara) na Isdore Shirima (Arusha), wakaamua kila upande uboreshe kwake,"alisema.

Akijibu malalamiko hayo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Shambarai Burka, Yohana Mollel, alisema japokuwa amefika hapo miaka ya karibuni ameukuta mgogoro huo, lakini majirani zao wanapaswa kuboresha soko na mnada wao ili wapate wateja.

"Siku hizi kuna kitu kinaitwa soko huria kwa kuamua kufanya biashara ya kuuza na kununua hivyo wana Simanjiro wajipange kuvutia wateja," alisisitiza Mollel.

# WWF yaridhishwa ongezeko la malipo kifuta jasho

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MFUKO wa Wanyamapori Duniani (WWF), limeeleza kuridhishwa na ongezeko la malipo ya kifuta jasho kwa wananchi wanaopoteza mazao yao, kutokana na kuharibiwa na wanyamapori, hasa katika wilaya zinazotishiwa na migogoro kati ya binadamu na tembo.

Msimamizi wa Mradi wa SOKNOT, ambaye pia ni mtaalamu mbobezi wa tembo, Prof. Noah Sitati, akizungumzia migogoro kati ya tembo na binadamu, alisema malengo yao ni kupunguza migogoro hiyo katika maeneo sita yaliyolengwa.

"Ukiangalia vile tumeona kwa miaka miwili ile inayoitwa consolation, ambayo inalipwa na serikali imeongezeka kwa kasi kubwa mno. Imeongezeka kutoka Sh. milioni 20 mpaka kufikia Sh. milioni 100 na kitu. Hii ni hatua nzuri na sisi wadau tunaridhishwa," alisema Prof. Sitati.

WWF ambayo inatekeleza mradi mkubwa wa SOKNOT katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro, imejitosa kutafuta suluhu ya kudumu ya migogoro, kati ya tembo na binadamu katika ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, kwa kuipunguza kwa asilimia 40 ifikapo mwaka 2025.

Mradi huo unalenga kulinda na kuhakikisha wanyamapori wanaovuka mipaka na kutembeleana kutoka Kusini mwa Kenya na Kaskazini mwa Tanzania, pia wanaendelea kupita kwenye mapito yao waliyokuwa wanapita zamani.

"Mkomazi ni moja ya maeneo yanayoongoza kwa migogoro kati ya tembo na binadamu nchini. Tembo wameongezeka kutoka 59 (2014) mpaka kufikia 1,200 (2019) kwa kipindi cha miaka mitano. Tembo amekuwa mnyama mharibifu na migogoro imekuwa mikubwa sana katika eneo la Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

"Mkomazi Ecosystem (ikolojia) ambayo inapakana na TSAVO (Hifadhi ya Taifa ya Kenya) kwa upande wa Kenya. Ukingalia ecosystem yetu ina tembo zaidi ya 16,000 upande wa Tanzania na Kenya ukijumlisha wote. Sasa ukiangalia ongezeko hilo ndio maana utaona migogoro imekuwa mingi katika wilaya sita za Mkinga, Korogwe, Lushoto, Same, Mwanga na Rombo." alisema.

Katika Wilaya ya Korogwe, wananchi wake wamepoteza mazao yao baada ya kuharibiwa na tembo waliovamia ekari 1,251.6

Ofisa Wanyamapori wa wilaya hiyo, Lina Nyange, alisema kwa mwaka 2022 tembo hao walivamia vijiji 18 na kuharibu ekari 612 zilizokuwa na mazao ya wakulima.

Kutokana na uharibifu huo, serikali imelazimika kuwalipa fidia au kifuta jasho, wananchi walipoteza mazao yao, zaidi ya Sh. milioni 123. 8.

Wakati katika Wilaya ya Mkinga, migogoro kati ya tembo na binadamu katika maeneo yaliyoko pembezoni mwa ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, imesababisha hasara kubwa kwa wakulima wake, baada ya tembo kuharibu mazao mbalimbali katika ekari 404.42 kwa kipindi kisichozidi miezi 12.

Akizungumzia migogoro hiyo, Kaimu Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Mkinga, Mamboya Buge, alisema mashamba hayo yaliyokuwa na mazao ya minazi, migomba, mihogo, mahindi, choroko, korosho, nanasi, mpunga, fenesi, mikaratausi na miembe, yaliharibiwa na tembo hao mwaka 2022.

Kwa mujibu wa Buge, idadi ya watu walioharibiwa mashamba yao kwa mwaka jana walikuwa 108, mwaka 2021 walikuwa watu 19, mwaka 2020 walikuwa 43, mwaka 2019 walikuwa 12, mwaka 2018 walikuwa 14 na mwaka 2017 walikuwa 28.





## Akamatwa madai kujiunganishia maji kinyemela

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

MKAZI wa Mtaa wa Nyakato Kata ya Nyasubi, Samwel Samson, anashikiliwa na Jeshi la Polisi Wilaya ya Kahama kwa tuhuma ya kujiunganisha maji bila kufuata utaratibu na kuyatumia katika shughuli za umwagiliaji wa bustani ya mboga.

Inaelezwa kuwa mtu huyo alikuwa akitumia maji hayo kwa muda mrefu kwa shughuli ya kilimo na mifugo, huku mengine akijaza katika kisima kilichopo ndani ya nyumba yake.

Hayo yalibainishwa juzi na Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mzingira Mjini Kahama (KUWASA), John Mkama wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kuwa taarifa za hujuma walizipata kutoka kwa wasamalia wema na walikuwa wakifuatilia kwa ukaribu ili kujua ukweli wake mpaka walipomkamata mtu huyo.

"Kitendo cha kuchepusha maji ni kosa kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ya Maji Namba 5 ya Mwaka 2019, hivyo mtuhumiwa anafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili kwa sasa tunasitisha huduma na upelelezi kwa ushirikiano na polisi.

Mtendaji wa Kata ya Nyasubi, Innocent Kapere, alikemea kitendo hicho kilichotokea katika eneo lake la utawala na kuwatahadharisha wananchi kuacha kujiunganisha huduma hiyo bila ruhusa ya KUWASA.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Elias Sitta alisema wanafahamu jirani yao kuwa ana bustani ya mboga na wao ni wateja wake licha ya kwamba hawakufahamu anapata wapi maji ya kumwagilia bustani hiyo.

Awali akihojiwa baada ya kukamatwa Samweli alikiri kuiba maji bila kufuata utaratibu na kwamba alifanya hivyo baada ya kuwa na uhaba wa maji kwenye kisima chake.

Alisema alianza kufanya hivyo miezi miwili iliyopita mpaka anakamatwa na mamlaka na sio kweli kuwa alianza mwaka jana kama wanavyodai majirani zake.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyakato, Hussein Mwita alieleza kuwa mtu anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa hatua zaidi za kisheria na watakapokamilisha upepelezi wao watamfikisha mahakamani na kuwataka wananchi kuacha vitendo hivyo kwa vinahujumu mamlaka na kuipotezea mapato yake.

# TBS yawanoa wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Ziwa, limetoa mafunzo kwa wafanyabiashara, waagizaji na wazalishaji wa vifaa vya ujenzi jijini Mwanza ili kuwajengea uelewa kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya udhibiti ubora wa vifaa hivyo.

Akifungua mafunzo juzi, Kaimu Katibu Tawala Mkoa Mwanza, Emil Kasagala aliwataka wafanyabiashara hao kuwa wazalendo kwa kuagiza na kuzalisha vifaa vyenye ubora na vinazokidhi viwango vya TBS kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Alieleza kuwa serikali inatarajia kuona vifaa vinazoingizwa sokoni vinakidhi ubora wa kimataifa ili kuleta tija kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wananchi pamoja na ile ya kimkakati ikiwemo Daraja la Kigongo- Busisi pamoja na meli mpya ya Mv.Mwanza.

Ofisa Usalama wa Chakula TBS, Kanda ya Ziwa, Nuru Mwasulama alisema mafunzo hayo ni mwendelezo wa kutoa elimu kwa umma kuhusu ubora wa bidhaa na vifaa mbalimbali kulingana na sheria na viwango vilivyowekwa na TBS hatua itakayosaidia kuondoa sokoni bidhaa na vifaa vilivyo chini ya kiwango.

"Lengo ni Watanzania kuwa na uelewa wa kuhoji mambo ya msingi kuhusu ubora wa bidhaa na vifaa vilivyothibitishwa na TBS ndiyo maana tunaendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali," alisema Mwasulama.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema utolewaji wa elimu ya namna hiyo mara kwa mara utasaidia wafanyabiashara kufuata miongozo ya serikali pamoja na TBS ili kuepusha kukamatwa na bidhaa iliyochini ya ubora.



Shekhe wa Mkoa wa Shinyanga, Ismail Makusanya akiongoza Swala ya Eid Al Adha katika viwanja vya Sabasaba, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wajane wakumbushwa kuchangamkia fursa za mikopo

**Na Alex Sayi,** MASWA

MKUU wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge amewataka wajane wilayani Maswa mkoani Simiyu kuchangamkia fursa za mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri hiyo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kujikwamua kiuchumi.

Alitoa kauli hiyo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani yakiwa na kauli mbiu isemayo 'Wezesha wajane kwa teknojia bora, kuwainua kiuchumi'. Kaminyoge alisema kuwa serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuweka mikakati ya kukabiliana na kero za wajane kwa kuimarisha mifumo ya kulinda haki zao kwa kutungwa Sheria za Msaada wa Kisheria No.1 ya Mwaka 2017.

Naye Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa,David Ntinginya alisema kuwa serikali imewezesha kutungwa kwa Sheria ya Ardhi ya Kijiji Namba 5/1999 kifungu cha 20 (1) ambacho kinatoa nafasi kwa wanawake wakiwemo wajane kumiliki ardhi na kueleza kuwa wamejipanga kutoa msaada wa kisheria kwa wanawake hao bure.

Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii wilayani humo, Rodgers Limo alisema kuwa maadhimisho hayo yamewakutanisha wajane 400 kutoka maeneo tofauti, huku wilaya hiyo ikikadiwa kuwa kuna na wajane 8,000. Mwenyekiti Mteule wa Shirikisho la Wajane Wilaya ya Maswa, Carloline Shayo alisema kuwa wajane wamefurahi kukutana na wanasheria ambao wanatambua haki za wajane na kusema kuwa ujane una changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na kutengwa na jamii.

# Kampuni yatoa msaada wa vyoo shule ya sekondari

**Na Mwandishi Wetu,** SENGEREMA

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya Sotta Mining Corporation Ltd, ambayo inajenga mgodi wa dhahabu wa nyanzaga imekabidhi vyoo vipya 12 kwa Shule ya Sekondari Busisi.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi vyoo hivyo, Mkurugenzi na Meneja Mkuu wa Sotta, Damien Valente alisema msaada huo ni kwa wanafunzi 496 wanaosoma shule hiyo pamoja na walimu wao ambao awali walikuwa wakitegemea matundu manne ya choo.

Alisema mpango upo chini ya udhamini kamili wa kampuni hiyo na ujenzi huo ulifanywa kwa kushirikisha wajenzi wa ndani na jamii kupitia Shirika la Wazalendo Group.


Valente alisema mpango huu ni mmoja katika shughuli nyingi zilizotekelezwa na Sotta ikiwa ni wajibu wa kampuni hiyo kwa jamii.

"Sotta Mining imejidhatiti kujenga biashara imara na ulimwengu bora, viungo viwili muhimu vya mafanikio ya muda mrefu na hapa leo tunashuhudia serikali na sekta binafsi vikifanya kazi pamoja kwa manufaa ya wanahisa wetu, waajiriwa wetu, washirika wetu wa kibiashara, kwenye jamii tunapoishi na kufanya kazi."

Naye Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Amani Tangalo, akizungumza wakati wa hafla hiyo aliishukuru kampuni hiyo kwa msaada huyo.

Kadhalika, alitumia nafasi hiyo kuwahimiza wanafunzi wa shule hiyo kutunza vyoo hivyo kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi wengine wa baadae katika siku zijazo.

SMCL ni mradi wa pamoja kati ya Tanzania inayomiliki asilimia 16 na kampuni ya uchimbaji madini ya Nyanzaga inayomiliki asilimia 84 ambayo ni kampuni tanzu ya OreCorp Tanzania Limited kwa ajili ya kujenga mradi wa Sh. trilioni 1.1 kusini mwa Ngoma katika Wilaya ya Sengerema kufuatia upatikanaji wa leseni maalum ya uchimbaji madini Desemba 13 mwaka 2021.




Ukurasa 13

Anayeikwaza NEMC anakwaza maisha yake

BUFE
IJUMAA JUNI 30, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

**Siku wakazi Nyamagana walivyochoshwa na kero barabara, waingia kazini kujitengenezea**

UCHUMI

# Uchumi Buluu unaowaunganisha 'kuwatoa' wanawake na vijana wa Pemba na Tanga

## •Wawekewa mtaji mezani waianze safari

**Na Beatrice Philemon**

MRADI wa Bahari Mali unaofadhiliwa na Ubalozi wa Ireland nchini, umekuja na jipya kwa mikoa ya Tanga na Kisiwa cha Pemba, wanawake na vijana wanajengewa uwezo kushiriki ujasirimali na uchumi wa buluu, vilevile kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi.

Kupitia mradi huo, wanawake na vijana watapewa elimu ya ujasiriamali washiriki katika biashara ya ufugaji viumbe maji kama vile kaa, majongoo bahari, ulimaji zao la mwani, chumvi, kupandaji mikoko majini, ufugaji nyuki na rasilimali za bahari.

Pia, ni mradi wa baharini utakaoanzisha programu atamizi kwa vikundi vitakavyoshiriki ujasiriamali wa uchumi wa buluu. Tayari kuna vikundi 19 vitavyonufaika kwa miaka mitatu, kila moja kikipatiwa mafunzo ya ujasiriamali na mtaji wa Euro 12,500 (sawa na shilingi milioni 32).

Imezindunduliwa mkoani Tanga na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, David Silinde, katika halfa iliyohudhuriwa na Balozi wa Ireland nchini, Mary O'neill; pia Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar,Dk. Aboud Jumbe.

Pia, walikuwapo wenyeviti wa halmashauri za Mkinga na Pangani, Mkuu wa Wilaya ya Micheweni Pembana wadau wa maendeleo na wawakilishi wa sekta binafs, mashirika yasiyo ya kiserikali, pamoja na wanufaika wa mradi.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, David Silinde, akimuangalia kaa katika maonyesho yaliyoandaliwa na wanufaika wa mradi kutoka Pemba na Tanga wakati wa uzinduzi wake, mkoani Tanga. **PICHA: BEATRECE PHILEMON.**

Meneja Mradi wa shirika la kimataifa la IUCN, Elinas Monga, anaiambia Niopashe kuwa hadi sasa ubalozi wa Ireland Tanzania umetoa fedha Euro 1.8 million sawa na zaidi ya shilingi bilioni nne kwa shirika la IUCN, kutekeleza mradi.

Anasema Mradi wa Bahari Mali unalenga kukuza uchumi wa jamii ya pwani, hasa wanawake na vijana wakijengewa uwezo wa kukabiliana na mabadiliko tabianchi.

" Kwa kuanza, jumla ya shilingi milioni 192 zimetolewa na shirika la IUCN kwa vikundi sita ili waweze kuanzisha miradi mbalimbali ya uchumi wa buluu katika mkoa wa Tanga na Kisiwani Pemba," anasema.

**NAIBU WAZIRI MIFUGO**

Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, David Silinde anasema mradi unakusudia kuboresha uhifadhi wa mifumo ikolojia ya bahari kwa kuboresha usimamizi hasa ngazi za jamii.

Anaitaja ni jambo muhimu kwa sababu uchumi huo wa buluu ikigusa uvuvi na utalii wa pwani, unategemea huduma za ikolojia baharini kama vile matumbawe (coral reefs), mikoko (mangroves) na na majani baharini.

Hivyo, katika kuboresha taasisi za kijamii zinazosimamia rasilimali bahari kama vile BMU, inaweka umuhimu kwa nchi kufaika na fursa za uchumi wa buluu kwa muda mrefu.

Pia, anashauri taasisi ya serikali ya uhifadhi wa maeneo ya Bahari (MPRU), kuanza kufikiria kuhifadhi maeneo makubwa ya bahari kwa njia shirikishi, tofauti na uhifadhi wa maeneno madogo wa sasa.

Kuhifadhi maeneo makubwa baharini anasema kunaruhusu matumizi mchanganyiko, hata kuifanya rasilimali bahari za nchi kuwa chini ya uangalizi maalumu, tofauti na sasa sehemu kubwa haina usimamizi.

Lengo la Umoja wa Mataifa unahitaji kuhifadhi asilimia 30 ya eneo la bahari kufikia mwaka 2030, ili kukabili upotevu wa baionuai na mabadiliko ya tabianchi, ikijenga uchumi imara na stahimilivu.

Silinde anaushukuru ubalozi wa Ireland nchini, kwa kushirikiana na serikali hasa katika sekta ya mifugo.

Hasi sasa tafiti zinaonyesha changamoto kubwa waliyonayo wananchi wa Pwani katika kutumia rasilimali za bahari kibiashara ni ukosefu wa maarifa ya biashara na mitaji.

"Serikali kupitia Wizara ya Mifugo wa Uvuvi imeliona hili na katika bajeti ya wizara ya mwaka 2022/2023 serikali imetenga fedha kwa ajili ya kutoa mikopo isiyokuwa na riba kwa vikundi vya kijasiriamali kwenye sekta ya uchumi wa buluu, "anasema waziri.

**TANGA NA PEMBA**

Mradi unatarajiwa kufanya uragibishi kuhakikisha jamii na wadau wa uchumi wa buluu, wanapata uelewa ili uwe endelevu kuhifadhi maeneo ya bahari na pwani.

"Hakuna namna tunaweza kuhifadhi bahari na mazingira ya pwani tusiyoyafahamu vizuri na hakuna namna tunaweza kuwa na mipango mizuri ya uchumi wa buluu bila kuwa na taarifa na maarifa ya kutosha, ni tafiti pekee zinazoweza kutusaidia," anasema Silinde.

Anaziomba sekta binafsi ziwekeze katika eneo hilo la uchumi wa bluu, kwa sababu ufugaji viumbe maji umekua, ikiwamo jamii illivyohamasika kwa biiashara ya ufugaji viumbe maji kama kaa na majongoo bahari, pia sehemu kubwa inashughulika na ulimaji wa mwani.

"Hata hivyo kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa mbegu, vyakula na ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya ufugaji wa vi-

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

# Siku wakazi Nyamagana walivyochoshwa na kero barabara, waingia kazini kujitengenezea

## • TARURA washtuka, kazi ndio 'inaishia' waahidi 'tutaungana'

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

NI kazi ya pamoja wananchi wa Mtaa wa Kagomu Kata ya Mahina Wilaya ya Nyamagana, jijini Mwanza,wameamua kuondokana na adha ya hali mbaya ya barabara, wakifanya ujenzi wa barabara ya Mtaa wao kwa kiwango cha moramu.

Inaelezwa ni barabara yenye urefu wa zaidi ya kilomita moja inayounganisha barabara za shule ya sekondari katika kata ya Mahina, ili kuwaondolea kero zinazowakabili kwa muda mrefu, tangu mwaka jana magari hayapitiki, hali wanayolalamika inawakwamishia maendeleo yao.

Hao wakaunganisha nguvu zao na vitendea kazi vya majembe ya mkono, mabeleshi, sululu za kuchimba mitaro ya kupitisha maji, wakidai kuchoshwa na kero ya ubovu wa barabara.



Wananchi wa Mtaa wa Kagomu Kata ya Mahina Wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza, wakishiriki kujenga barabara kwa kiwango cha moramu. **PICHA ZOTE:ANTHONY GERVAS.**

**WENYE MTAA**

Mwenyekiti Mtaa wa Kagomu,George Peche anaeleza katika ujenzi huo, wakazi zaidi ya 100 wamejitokeza kushiriki, wakiwamo wadau waliochangia vifaa vya ujenzi kama vile saruji na matofali ya kujenga mitaro ya maji.

Peche anasema barabara hiyo imekuwa kikwazo cha muda mrefu kwao na tangu mwaka jana haipitiki, huku akiiomba serikali iwaunge mkono ujenzi, kazi waliyotarajia kukamilika mwezi huu.

"Ujenzi wa barabara hii utakuwa wa kihistoria ya pekee, kwa sababu wananchi wenyewe wamehamasika kufanya maendeleo ya mtaa wao, wakitumia zana za mikono.

"Wamejiwekea sheria kali, mtu ambaye hashiriki atakuwa akitozwa faini ya shilingi 5,000 kila anapokosa kuja, wakiwamo wageni wanaohamia," anasema Peche.

Pia anafafanua wakati akiingia madarakani mwaka 2019, alikuta barabara nyingi za mtaa wake hazipitiki, hivyo uliofuata 2020, akajitolea kutafuta greda la Halmashauri ya jiji la Mwanza, akiweka mafuta kwa gharama yake, akaitengeneza barabara maeneo manane yanayounda mtaa huo.

Hapo anadokeza kuna malalamiko ya wananchi, kwamba wanaishi katika makazi hayo, pasipokuwa na hati za viwanja.

Mkazi Alphonce Gabriel, anadai barabara zote za mtaa huo sio rafiki, hivyo zinatakiwa kuboreshwa au kujengwa na serikali kwa kiwango cha lami, akitoa na mfano linganishi kama ilivyo kwa Halmashauri ya Manispaa Ilemela.

Mchungaji wa Kanisa la Chrisco lililopo Kagomu Denis Boaz, anaiomba serikali kuunga mkono juhudi za ujenzi wao kwa kiwango cha moramu, wakati wakiisubiri serikali kuwajengea lami baadaye barabara zote za mtaa huo, akisema hata hatua yao ya ujenzi haijulikani serikalini.

Mwashamba Shaban,mkazi wa Mtaa wa Kagomu, anataja changamoto hiyo ya barabara,iko na shida pacha ya maji hata kugeuka kwao mateso, kwamba kuyapata maji ya bomba ni sharti kwao kulipa shilingi 100 kutoka mifumo mbadala, ilhali jirani katika Manispaa ya Ilemela, yapo maji bomba.

Anasema kinamama mtaa huo wa Kagomu kata ya Mahina wana shida kubwa ya maji bomba,wakati Serikali ni ile ile ya Nyamagana na Ilemela wao wanapata maji bomba, pia barabara zao zimejengwa kwa kiwango cha lami,

"Kwetu huku tuna barabara kuu moja ya vumbi kutoka mjini hadi kata yetu Mahina, ambayo magari ya daladala ikifika saa 12 jioni kurudi nyumbani usafiri ni shida, kupata mpaka upande bajaji au bodaboda shilingi 5,000 hadi shilingi,8,000.

"Tunaiomba Serikali ituangalie kwa jicho la huruma kinamama Kagomu tupate barabara kuu ya lami na maji bomba ya uhakika," anatamka Mwashamba.

Nipashe ilipotaka ufafanuzi wa Mwenyekiti wa Mtaa Peche, kuhusu upana wa shida hiyo, akajibu:"Ni kweli mtaa wangu una shida kubwa ya maji yanatoka mara moja au mara mbili kwa wiki.

Hiyo inatajwa ni changamoto kubwa, kwa kinamama wanaolazimika kutembea umbali wa kilomita tatu hadi nne kufuata maji bomba, ndoo moja wananunua shilingi 100 hadi 200 hasa wakati wa kiangazi."

Anasema wanaitegemea serikali kuwasogezea huduma ya maji upitia chanzo kikuu cha maji cha mradi mkubwa unaotoka Butimba,ili kuwasaidia wananchi kuondokana na shida hiyo.

**TARURA YAFAFANUA.**

Kaimu Meneja Wakala wa Barabara Mijini na vijijini (Tarura) wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza, Mhandisi Malulu Lukenza, anaunga mkono juhudi za wananchi wa Mtaa wa Kagomu kujenga barabara kwa nguvu zao wenyewe.

Mhandisi Lukenza anafafanua kinachofanyika TARURA ni kwamba: "Kwa hadhi ya jiji ni kweli barabara zote za mitaa wilaya Nyamagana zinatakiwa kujengwa katika kiwango cha lami. Lakini, tuna ufinyu wa bajeti, mfano mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetoa shilingi bilioni 4.5 tu kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo."

Anataja mtandao wa barabara zote Nyamagana, ni jumla ya kilomita 1,025.612, sawa na urefu wa kutoka Mwanza hadi Dar-es Salaam, zikiwa katika mpango wa kujengwa kiwango cha lami, ila bajeti yao ya kujenga ni finyu, hivyo anaahidi watachangia ujenzi huo katika kiwango cha moramu.

Mhandisi Lukenza anasema barabara zinazotakiwa kujengwa kiwango cha lami ni kilomita 40.349; kiwango cha mawe kilomita12.939; changarawe kilomita 69.902; zege kilomita 7.481; na udongo kilomita 894.941, lakini kwa sasa bajeti yao haikidhi mahitaji yote ya ujenzi.

Katika kusaidiana, Mhandisi Lukenza anashauri kinachotakiwa viongozi wa eneo hilo waandike barua ya kutoa taarifa ya ujenzi kama kumbukumbu ya baadaye, ila TARURA kupitia wataalamu wake, wataenda kukagua ujenzi na kuwaongezea nguvu, ili kazi iwe na ubora zaidi.

Hata hivyo, Nipashe ikabaini kuwapo barua ya aina hiyo iliyoandikwa mnamo Mei10 mwaka jana kutoka kwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Kagomu kuhusu kero ya barabara.

Mhandisi Lukenza anaahidi wataalamu wa TARURA watashirikiana na wananchi kusimamia ujenzi, ikiwamo katika kuzingatia michoro, kuweka karavati za kupitisha maji na makadirio ya bajeti ya ujenzi huo hadi kukamilika.

Anasema barabara nyingi zilizopo zimekuwa zikijengwa chini ya usimamizi wao kwa kutumia greda la jiji na ushirikiano wa nguvu za wananchi.

Vilevile anataja barabara zingine kwenye mpango wa ujenzi wa kiwango cha lami ni Buhongwa-Kishiri-Igoma, zinazotarajiwa kuanza kujengwa kuanzia mwezi Agosti ijayo, zitakazogharimu kiasi cha shilingi bilioni 12; nyingine zilizopo kwenye bajeti ya 2023/24 ni Mkuyuni,Mahina Kati, Nyakato, Bismarck, Mwananchi na Alliance.

**MIKAKATI UMEME**

Katika eneo la umeme, Mwenyekiti Peche anajigamba ameweza kuwasaidia wananchi kupata huduma za kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mwanza kwa baadhi ya kaya zilzokuwa zikiishi gizani, ikizingatiwa gharama rasmi za kuunganishiwa ni shilingi 321,000.

Anaeleza kuwa Mtaa wake una zaidi ya kaya 1,180 na kati yao kuna kaya 300 hazijapata huduma ya umeme na zinaishi gizani, hivyo yuko katika mapambano kuhakikisha zinaunganishiwa huduma hiyo kutoka mradi wa Wakala wa Umeme Mijini na Vijijini (REA ).

**ENEO LA AFYA**

Peche anasema wameshapata shilingi milioni 170 kati ya shilingi bilioni moja, zitakazotolewa kujenga Kituo cha Afya Mahina. Fedha za sasa zilitolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii,(TASAF) na kazi ilikwishaanza.

Vilevile, kuna kazi ya ujenzi wa ofisi ya Mwenyekiti wa Mtaa, itakayogharimu shilingi milioni 48, ambazo wananchi wamechangia nguvu kazi, ikiwemo fedha na Mfuko wa Jimbo kutoa shilingi milioni tano.



TAFAKURI YA MLALAHOI

# Anayeikwaza NEMC anakwaza maisha yake






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

BANGI ni mmea unaochukiwa na wengi kwa kuwa ni dawa za kulevya zinazoathiri akili ya mtumiaji, ingawa kuna wanaoamini kwamba huwaongeza akili, nguvu na maarifa.

Zamani hatukujua kuwa bangi inakatazwa mpaka hapo tulipopata makamo na kujua sheria za nchi, ndipo tukabaini kuwa kumbe mmea huo ni haramu.

Lakini baadaye tukaja kugundua, kuwa katika mataifa mengine hususan ya Ughaibuni, bangi hata madukani inauzwa na kununuliwa kama sigara au tumbaku nyingine ya kawaida.

Sasa nani aliharamisha bangi na kwa nini? Likawa ni swali, kwa sababu kama Ulaya bangi inahalalishwa na katika hata baadhi ya mataifa ya Afrika, kwa nini sisi iwe haramu?

Hivi bangi ilitufanya nini mpaka tuiharamishe? Ilimwua nani? Tukashangaa kwa nini nchini ilipigwa marufuku wakati ugenini ni halali? Katika nchi zingine tukaamini kuwa walichunguza wakabaini ina faida na hasara.

Kwetu tukaamini haraka tu kuwa haina faida hata kidogo. Tukashindwa kujishughulisha kidogo, kuamini kama inaweza kuwa na manufaa angalau kidogo na kuizima jumla, kwamba ni dawa za kulevya na ukionekana nayo ama zako au zao.

Kwa hiyo bangi ni bangi tu na sheria ya nchi inasema anayepatikana nayo akiitumia au kuiuza, adhabu ni pale pale ya kifungo au faini, kwa sababu ni mihadarati, mpaka hapo tutakapoaminishwa vinginevyo.

Na wanasema sheria ni msumeno, ukikata umekata. Hivyo tunatakiwa kuiheshimu na kuitii bila shuruti, kinyume chake kuna adhabu yake ya kutosha kabisa na haina mchezo.

Kama tumeamua kuheshimu na kutii sheria bila shuruti, basi tusipindepinde yanapokuja masuala yaliyo chini ya sheria na tuyafuate na kuyazingatia ili nchi iweze kusonga mbele.

Watanzania ni wazuri sana kuzungumzia utii wa sheria bila shuruti, lakini ni wazuri pia kupindisha sheria kwa shuruti au bila shuruti, wakiangalia muktadha na anaguswa nani wakati huo.

Tujiulize, hivi kwa nini hivi sasa kuna migomo ya hapa na pale katika maeneo mengi, mara wafanyabiashara wanagomea kodi, wengine hawakubaliani na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na sababu wanazo.

Kuna wengine wanaandamana maeneo yao ya biashara yamefungwa na Baraza la Taifa Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kutokana na mambo mbalimbali, kubwa likiwa ni la kelele.

Wanapobanwa wanaandamana na ghafla kigogo fulani anaibuka na anaamuru amri ya NEMC dhidi ya wafanyabiashara hasa wa baa. itenguliwe, eti kwa sababu inaathiri uchumi.

Hivi kwa jicho la haraka haraka, baa zilizofungwa katika maeneo husika ni zote au baadhi? Zilikiuka au hazikukiuka sheria ya NEMC ya uchafuzi wa mazingira kwa kelele na mitetemo? Kama ni zote, ina maana uchumi huo unachangiwa na wahalifu?

Hivi NEMC imeundwa kisheria au siyo na inavyofanya ni halali au haramu? Kwani baa bila muziki mkubwa inaacha kuwa baa? Nani alisema ili ulewe lazima upigwe muziki mkubwa?

Mbona zamani havikuwapo vipaza sauti vya kutolea mikelele kama haya ya leo, lakini bado watu walimwabudu Mungu wao kwenye nyumba za ibada na kujirudia nyumbani?

Zamani enzi hizo tulikuwa na baa za pombe za asili hakukuwa hata na redio, bali tulipolewa tulijiimbia nyimbo zetu na kurudi kujilalia. Ina maana Wakoloni ndio walituletea muziki mzito baa na mengineyo?

Nadhani wanaoona kuwa wenye baa wanaonewa kwa kufungiwa maeneo yao kutokana na kukiuka sheria za mazingira, wawatafutie maeneo mbali na makazi wakapigie makelele huko.

Kwani haiwezekani inayejali kodi itokanayo na ulevi, akatenga maeneo mahususi kwa ajili ya baa na watu wakajenga mbali, kama zilivyo dampo za taka tukazifuata kujirusha?

Kwa nini inashindikana kueleweka kuwa baa jirani na makazi ya watu, shule na hospitali ni kero kwa wazee, wanafunzi na wagonjwa? Maeneo kama hayo kunahitajika maduka madogo tu ya vinywaji, mtu anunue akanywee kwake.

Kwa maana hiyo, mtu anayetaka kulewa kwa kelele za muziki alazimike kufunga safari na kufuata baa mbali akaburudike, kisha arudi kwake usiku alale bila kusumbua wenzake.

NEMC iachwe itimize majukumu yake ya msingi iliyopewa kwa mujibu wa sheria na isiishie hapo, iguse pia wale wanaopita na mipaza sauti mitaani kualika mikutano ya wanasiasa na wanadini kwa sauti kubwa.

Inajulikana katika mazingira ya sasa ya biashara huria, maeneo mengi ya biashara yamekamatwa na viongozi waliojificha nyuma ya wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa.

Alamsiki!

UCHUMI

# Bodi ya Ujenzi yaja na angalizo la usajili mdogo, haja ya kuwatumia

**Na Yasmine Protace**

MAENDELEO ya Uchumi katika nchi yoyote ile, yanaletwa na wataalamu walio na sifa, ikiwamo katika sekta ya ujenzi.

Katika kuhakikisha miradi mikubwa inaendelezwa nchini Tanzania, sekta ya ujenzi imefanya makubwa katika ujenzi wa miradi ya kisasa.

Tanzania imo katika nchi barani Afrika zinazotekeleza miradi mikubwa, chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi hapo inatajwa barabara, madaraja, vivuko na majengo katika mikoa mbalimbali.

Kwa kulitambua hilo sasa, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi AQRB imekuwa ikitoa mafunzo endelevu ya wataalamu, lengo ni kuwanoa na kubadilishana uzoefu wa kitaaluma kwa mambo yanayowahusu Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi, ili kuboresha uwezo wao.

Kaimu Msajili wa Bodi ya AQRB Mkadiriaji Majenzi Nyaswa Kalomo, anasema hivi karibuni mkoani Morogoro, walikuwa na darasa ambalo lina mada kuu ya Usimamizi wa Miradi katika Tasnia ya Ujenzi Nchini.

Anazitaja mada ndogo zilizoambatana nazo ni kushughulikia madai na usuluhisho wa migogoro katika tasnia ya ujenzi nchini, pia mapitio kuhusu uzingatiaji kodi katika ujenzi kwa mujibu wa sheria yao.

"Tangu mwaka 2003 Bodi imekuwa na utaratibu wa kufanya semina za mafunzo endelevu kwa lengo la kuwanoa wataalamu waliosajiliwa na bodi ili kuwawezesha kuendana na maendeleo au mabadiliko ya sheria, sayansi pamoja na teknolojia yanayotokea ulimwenguni hivi sasa," anasema Kalomo.



Muonekano wa ujenzi wa barabara ya mabasi ya mwendo kasi ukiendelea katika eneo la Vingunguti kwenda Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Anaongeza kuwa, katika kipindi hiki hadi kufikia Mei 2023, imesajili jumla ya wataalamu 1,373, pia kampuni za kitaalam 456, akilalamika ongezeko hilo bado ni dogo.

Mkakati wao unataja kuongeza idadi ya wataalamu wanaosajiliwa kufikia 160 kwa mwaka, ikilinganishwa na wastani wa wataalam 60 kwa miaka minne iliyopita.

"Bodi imesajili orodha ya wahitimu 704 wakimaliza fani za ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi kwenye vyuo vikuu, lengo la orodha hiyo ni kuhakikisha wahitimu wote wanaosajiliwa na bodi baada ya kuhitimu masomo yao," anasema Mkadiriaji Majenzi Kalomo.

Anasema katika mwaka huu wa Fedha 2022/23, Bodi ilipanga kukagua miradi 3,120 kwa lengo la kuhakikisha wataalamu iliyowasajili wanahusishwa katika ubunifu usanifu, usimamizi wa kazi za ujenzi na ushauri.

Kalomo anataja Bodi ilifanikiwa kukagua miradi 3,889 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 25 ya lengo, akinena: "Mwaka 2006 Bodi ilianzisha mpango wa mafunzo kwa vitendo wa wahitimu wa vyuo vikuu kutokana na jitihada za wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kufadhili mafunzo hayo.

"Uwezo wa Bodi kutoa mafunzo kwenye programu ya EAPP umeongezeka kutoka wahitimu 39 miaka mitano iliyopita hadi kufikia wahitimu 126 mwaka huu," anasema.

**MWENYEKITI WA BODI**

Mwenyekiti wa Bodi hiyo Dk. Ludigija Bulamile, anasema kumekuwapo idadi ndogo ya wabunifu na wakadiriaji majenzi, wabunifu wa ndani, wabunifu wa mandhari ya nje wasanifu teknolojia ya majengo, watathmini majengo, wasimamizi wa ujenzi na wasimamizi wa miradi wanaoajiriwa na serikali.

Dk. Ludigija anasema uhaba huo wa huduma katika miji na vijiji, zimekuwa zikisuasua, hata anaiomba serikali kuendelea kuajiri wataalamu waliosajiliwa na bodi katika ofisi zote za umma.

"Kila mmoja wetu ni shahidi kuwa serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imekuwa ikitekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, hivyo Bodi inashauri ushirikishwaji wa wataalamu wa ndani ni muhimu, ili matengenezo ya hapo baadaye yasije kutegemea wataalamu kutoka nje,' anasema Dk. Bulamile.

Anakumbusha taasisi za umma ni miongoni mwa wadau wakubwa wa uendelezaji wa sekta ya ujenzi hivyo serikali kupitia sheria ya manunuzi ya umma PPRA imeruhusu Taasisi nunuzi kutumia wataalamu wake wa ndani kwa lengo la kuipunguza gharama za utekelezaji wa miradi.

Hata hivyo, serikali imeshaziagiza mamlaka za usimamizi kuhakikisha wataalamu wanaopewa dhamana ya kutekeleza miradi wanazingatia sheria za kodi ili serikali iweze kupata mapato na shughuli za ujenzi ziendelee kutoa mchango katika ukuaji wa uchumi.

Katibu Tawala Msaidizi,Miundombinu wa Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Ezron Kilamhama kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo anasema katika baadhi ya miradi ya ujenzi inayosimamiwa na kutekelezwa na wataalamu wa ndani ukwepaji wa kodi umekuwa mkubwa kiasi cha kusababisha malalamiko dhidi ya umahiri na ujuzi wa kampuni za ndani.

# Uchumi Buluu unaowaunganisha 'kuwatoa' wanawake na vijana wa Pemba na Tanga

**INATOKA UK. 11**

umbe maji," anasema

**UCHUMI BULUU VS UVUVI**

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Zanzibar, Dk. Aboud Jumbe, anasema uzinduzi wa mradi wa Bahari Mali ni tukio muhimu kwa Wazanzibari, kwa sababu Zanzibar inategemea bahari kwa asilimia 29 ya uchumi wake, hivyo serikali yake inaweka msisitizo kutumia rasilimali bahari kwa njia endelevu, kunufaisha sasa na baadae.

Hadi sasa Zanzibar ina sera na mkakati unaosimamia dira ya Rais Dk. Hussein Mwinyi, iliyomo katika Maono ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, inayosisitiza uchumi wa buluu kama nguzo muhimu ya kukuza uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya watu wake.

"Ni vizuri pia tukawa na uelewa wa pamoja kuwa uchumi wa buluu haumaanishi tu shughuli za kiuchumi ila pia uhifadhi wa maeneo ya bahari na pwani, hasa mifumo muhimu ya ikolojia kama matumbawe, mikoko na majani bahari," anasema.

Programu ya sasa anaitaja inawajengea uwezo wananchi hasa kina mama na vijana katika ujasiriamali endelevu wa uchumi wa buluu, pia kuhifadhi maeneo baharini na pwani.

"Kabla ya kuzindua mradi Zanzibar tulishiriki katika kutoa maoni ya uandaaji wa mradi huu wa Bahari Mali, hivyo tuko tayari kushirikiana ," anasema.

**RC TANGA**

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, anaishukuru serikali ya Ireland kuleta mradi huo Tanga, akinena: "Tumejipanga vizuri namna ya kutumia rasilimali bahari. Sisi ni matajiri wa miti ya mikoko, miti hii inavutia sana nyuki kwa hiyo wananchi wa Tanga wanaweza kutumia miti hii na kujikita kwenye ufugaji wa nyuki."

Pia, anataja mradi huo utaongeza utalii kati ya Pemba na Tanga na utawala bora katika usimamizi wa rasilimali bahari, akiwa na mbiu "naomba wakazi wa Tanga kutumia fursa zinazotumia uchumi wa bluu."

Mkoa wa Tanga ni mdau wa kushirikiana na shirika la IUCN na wengine katika utekelezaji mradi huo.

**MNUFAIKA KUTOKA PEMBA.**

Fatma Larali kutoka kikundi cha Uvumbuzi Cooperative, Wilaya ya Mkoani Pemba, anasema hadi sasa wamejikita katika uzalishaji chumvi na kilimo cha mboga kama vile bilinginya, mchicha, pilipili boga, tungule.

Huku akishukuru mdau IUCN, anadema hadi sasa wana mabwawa manne kwa ajili ya kilimo cha uzalishaji wa chumvi na mashamba 5 kwa ajili ya kilimo cha mbogamboga.







Sehemu ya watoto walioshiriki swala ya Eid El Adha katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askari 667 Magereza wapandishwa vyeo, wapewa neno

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMISHNA Jenerali wa Jeshi la Magereza nchini, Mzee Ramadhan Nyamka, amewaagiza askari 667 waliopandishwa vyeo wasibweteke badala yake watekeleze majukumu yao ipasavyo ili kuleta tija ndani ya jeshi hilo.

Akizungumza katika hafla ya kupandishwa vyeo askari hao jana makao makuu ya Jeshi hilo, Kamishna Nyamka alisema kupandishwa vyeo kwa askari hao siyo kupunguziwa majukumu bali ni kuongezewa majukumu zaidi ya kiutendaji.

Alisema wanapaswa kujituma ikiwamo kuongeza ufanisi katika majukumu ambayo wamekabidhiwa na Jeshi hilo ili kazi yao ionekane ndani ya jeshi hilo na mbele ya jamii. "Nyie askari mliopanda vyeo mkafanye kazi kwa bidii ili mzidi kupanda vyeo, hiki cheo kisiwafanye mkawe wavivu na kubweteka badala ya kuchapa kazi,"alisema.

Hivyo, aliwataka kuendeleza nidhamu waliyonayo katika kazi kwa sababu nidhamu ndio inamuwezesha askari kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Awali, Kamishna wa Utawala na Rasilimali watu wa Jeshi hilo (DCP) Jeremiah Katungu, aliwahimiza askari waliopandishwa vyeo hivyo kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuleta matokeo chanya kwa Jeshi na taifa kwa ujumla.

"Naomba mkatekeleze majukumu mlilokabidhiwa na serikali ipasavyo msiende kubweteka baada ya kupandishwa vyeo,"alisema DCP Katungu.

Alisema asingependa kuona askari hao wanaishia vyeo hivyo badala yake wafanye kazi kwa bidii ili wazidi kupanda vyeo vingine.

# TRA Singida imefanikiwa kukusanya bil.11/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Singida, imefanikiwa kukusanya Sh.bilioni 11.89 sawa na ufanisi wa asilimia 96.4 ya lengo walilojiwekea la kukusanya Sh.bilioni 12.3 katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022.

Meneja Msaidizi TRA anayeshughulikia madeni, Hassan Mzee, aliyasema hayojana wakati akitoa taarifa ya makusanyo kwenye kikao kilichowajumuisha wafanyabiashara na wadau mbalimbali wa kodi.

Alisema kiasi hicho kilichokusanywa ni sawa na ukuaji wa asilimia 14 ya makusanyo ya mwaka 2020/2021.

Mzee alitoa mchanganuo kuwa katika kodi ya moja kwa moja malengo yaliyokuwa yamewekwa ni kukusanya Sh.bilioni 9.9 lakini zilizokusanywa ni Sh.bilioni 9.904 sawa na ufanisi wa asilimia 106, kodi zisizo za moja kwa moja zilikusanywa Sh.bilioni 1.9 sawa na asilimia 71.5 ya lengo lililowekwa la kukusanya Sh.bilioni 2.7.

Alisema kwa upande wa kodi za matangazo lengo lililowekwa ilikuwa ni kukusanya Sh.milioni 308 lakini walikusanya Sh.milioni 6.9 sawa na asilimia 2.2 na kodi ya forodha zilikusanywa Sh.milioni 9.2 sawa na asilimia 385 ya lengo lililokuwa limewekwa la kukusanya Sh.milioni 2.4.

Mzee alisema makusanyo kwa wilaya za kikodi ni kwamba kwa Wilaya ya Singida inayojumuisha Ikungi na Singida Vijijini iliwekewa lengo la kukusanya Sh.bilioni 9.5 lakini zilizokusanywa ni Sh.bilioni 9.8 sawa na ufanisi wa asilimia 103.

Alisema kwa Wilaya ya Manyoni ambayo inajumuisha na Itigi iliwekewa lengo la kukusanya Sh.bilioni 1.9 lakini zilizokusanywa ni Sh.bilioni 1.3 sawa na asilimia 71, Wilaya ya Iramba ambayo inajumuisha na Mkalama ilikusanya Sh.milioni 706.8 sawa na ufanisi wa asilimia 84 ya lengo la kukusanya Sh.milioni 841.

Alisema baadhi ya sababu za kutofikia ukusanyaji wa asilimia 100 kwa mkoa ni kushindwa kusajili wafanyabiashara wengi kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwani wengi hawako vizuri kwenye kutoa stakabadhi za EFD.

"Sheria iliyopo ni kwamba ili uweze kumsajili mtu katika VAT lazima awe anafikia mauzo ya zaidi ya Sh.milioni 100 lakini wengi hawafikii katika kiwango hicho na wanajitahidi wasiweze kufikia ili wasisajiliwe, hiyo ndio changamoto kubwa," alisema.

Mzee alitaja sababu nyingine ni kutokuwepo kwa viwanda mkoani Singida ambavyo vinazalisha bidhaa ambazo zinalipa ushuru wa forodha kwasababu ndio zinazotoa kodi ya moja kwa moja na nyingine ni malipo ya kodi za majengo kuingia moja kwa moja makao makuu bila kupitia mkoa husika. Mkuu wa Mkoa wa Singida,

Peter Serukamba, aliwataka wafanyabiashara kujenga utamaduni wa kulipa kodi, kutoa lisiti na kufanya biashara halali ili nchi iendelee.

Pia aliiagiza TRA kukutana na wafanyabiashara ili kurasimisha biashara zao kwani serikali inataka kuona kila mtu analipa kodi na ambayo ni halali.

Shekhe wa Mkoa wa Singida, Nassoro Issa, alisema hakuna nchi inayoweza kuendelea kama wananchi wake hawalipi kodi na kuwaomba wananchi kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

# Mbunge awatoa hofu wenye ulemavu kuhusu bandari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Khadija Taya amesema mageuzi yatakayofanyika katika Bandari ya Dar es Salaam yataleta manufaa kwa Watanzania ikiwamo watu wenye ulemavu.

Aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya chakula cha mchana na viongozi wa watu wenye ulemavu aliyoiandaa ili kuwa na mwamko wa kuchangamkia fursa zilizopo kwenye maeneo yao.

Alisema watu wenye ulemavu wasitishwe na maneno yanayozungumzwa kwa mageuzi ya bandari yatakayofanywa na Kampuni ya DP World, kwamba yanalenga kuleta tija kwa nchi na kuifungua kiuchumi.

"Hakuna sheria nchini inayoruhusu bandari kuuziwa mgeni nimekuja kuzungumza nanyi mfahamu bandari itakuza mapato ambayo yatasaidia ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii zinazotugusa wote,"alisema.

Aidha, alisema zipo fursa nyingi za watu wenye ulemavu za kujikwamua kiuchumi wanazopaswa kuzichangamkia ikiwamo iliyopo kwenye sheria ya ununuzi wa umma inayowapa fursa ya asilimia 30 ya zabuni kwa makundi maalum wakiwamo wenye ulemavu.

Aliomba kukimbilia fursa hiyo ili wajikwamue kiuchumi kwa kusajili kampuni na kupata zabuni kupitia sheria hiyo.

"Kuna zabuni ya masuala ya usafi ambayo haihitaji mtaji mkubwa sana, tunaomba taasisi za fedha ziwawezeshe mitaji ili kupata zabuni za kufanya kazi za serikali watu wenye ulemavu,"alisema.

Kadhalika, alisema kilichomsukuma kuzungumza na viongozi hao ni kutokana na serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuwakwamua kiuchumi, kukuza ujuzi lakini mwamko wa watu wenye ulemavu kushiriki katika fursa hizo umekuwa mdogo sana.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema serikali inaendelea kuweka fursa mbalimbali kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa kuwawezesha kufanya ujuzi na bunifu kwa kuwajengea vyuo vya ufundi.

Alibainisha kuwa serikali imetenga Sh.bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya watu wenye ulemavu kwenye mikoa ya Kigoma, Songwe na Ruvuma.





Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti la Kawetere linalomilikiwa na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), Arnold Shoo (kulia), akitoa maelekezo kwa maofisa wa wakala huo, wakati wa utoaji wa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa wananchi wa kata za Nsalaga jijini Mbeya na Ruiwa ya wilayani Mbarali juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Waishukuru serikali kurekebisha mpaka Hifadhi ya Ruaha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wanaoishi kando ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, wameishukuru serikali kwa mchakato unaondelea wa kurekebisha mpaka wa hifadhi hiyo ambao unalenga kuziondoa zaidi ya hekta 74,000 kwenye hifadhi.

Wananchi hao wametoa shukrani hizo kwa serikali ikiwa ni siku chache baada ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kutembelea mpaka huo wilayani Mbarali kwa nia ya kujiridhisha na mapendekezo ya marekebisho yanayotaka kufanyika. Aidha, hivi karibuni Bunge liliridhia mapendekezo ya marekebisho ya mpaka huo yaliyowasilishwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa.

Mapendekezo hayo yalianzishwa na kamati maalumu ya Mkoa wa Mbeya ambayo iliundwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kisha kuridhiwa na timu ya mawaziri nane wa kisekta ambao walikuwa wanashughulikia migogoro ya ardhi.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi wa Kitongoji cha Mwashikamile kilichopo katika Kata ya Luhanga, wananchi hao walisema mgogoro wa mpaka baina yao na hifadhi umedumu muda mrefu.

Mmoja wa wananchi hao, Amina Yohana alisema mgogoro huo ulikuwa unawafanya washindwe kufanya shughuli zao kwa amani lakini mpaka huo ukirekebishwa watakuwa na amani. Alisema kitongoji chao ni miongoni mwa maeneo machache ambayo wanatakiwa kuondoka lakini wana amani kwa sababu kuna maeneo ambayo yanabaki nje ya hifadhi na hivyo watakwenda kuishi huko.

"Tunaishukuru serikali kwa sababu kwa muda mrefu tulikuwa tunahangaika na mgogoro huu, lakini sasa hivi mpaka umewekwa vizuri na viongozi wamekuja mara nyingi kuja kutuelimisha tumeelewa," alisema Amina.

Naye Joseph Chuya aliiomba serikali kuwalipa fidia mapema ili waondoke kabla ya msimu wa kilimo haujafika ili kuondoa mgogoro mpya ambao unaweza ukaibuka watakapokuwa wanaondolewa.

Alisema msimu wa kilimo ukifika watatakiwa kuendelea kulima mazao mbalimbali kwa ajili ya chakula na hivyo wasipolipwa fidia wanaweza wakaendelea kulima kwenye maeneo hayo ambayo wanaishi kwa sasa.

Akizungumza wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge, Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Mkoa wa Mbeya, Syabuni Mwaipopo ambaye alikuwa mwenyekiti wa timu ya mkoa alisema walizingatia vitu mbalimbali wakati wanarekebisha mpaka huo.

Alivitaja baadhi ya vigezo kuwa ni pamoja na kuangalia maeneo yenye ardhi oevu, maeneo ya vyanzo vya maji, mwinuko kutoka usawa wa bahari, uoto wa eneo husika hasa wenye matete na magugu pamoja na kuangalia shughuli za kibinadamu. "Kuna baadhi ya maeneo ambayo ilikuwa lazima wananchi waondoke kabisa ili kulinda hifadhi, kuna shamba la madibira namba mbili ambalo limeungana moja kwa moja na Bonde la Ihefu hili ilikuwa lazima libaki kuwa sehemu ya hifadhi," alisema Syabumi.

Akizungumza na wananchi wa Kitongoji cha Mwashikamile, Waziri wa Maliasili, Mchengerwa alisema lengo la serikali ni kulinda maeneo yote ya hifadhi pamoja na kumaliza migogoro kati ya wananchi na hifadhi.

Alisema wanatekeleza mambo hayo kutokana na maelekezo waliyopewa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wanamaliza migogoro baina ya wananchi na hifadhi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Timotheo Mzava alisema kamati hiyo ilikwenda katika maeneo hayo kwa lengo la kujiridhisha na mipaka mipya inayopendekezwa kabla ya kufanya maamuzi.

Mwishoni mwa mwaka jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitangaza kuwa serikali ina mpango wa kurekebisha mpaka wa hifadhi hiyo kwa kufuta Tangazo namba 28 la Mwaka 2008 (GN. 28).

# ACB, Benki ya Malawi washirikiana kuimarisha mtaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UHUSIANO wa kidiplomasia wa kiuchumi kati ya Tanzania na Malawi, umezidi kuimarika baada ya Benki ya Akiba (ACB) kuingia makubaliano na Benki ya Taifa ya Malawi kukuza na kuimarisha mtaji.

Hayo yalisemwa juzi jijini Mbeya na Meneja Huduma Binafsi kutoka Benki ya ACB, Emmanuel Mseti wakati wa chakula cha jioni baina ya benki hiyo na wateja wake iliyolenga kutambulisha huduma zao mpya.

Aidha hafla hiyo ilikuwa na lengo la kusikiliza kero na maoni ya wateja kuhusu uboreshaji wa huduma zinazotolewa na benki hiyo. Mseti alisema uwekezaji huo umesaidia kuboresha huduma za kibenki pamoja na kuazisha huduma nyingine zinazokidhi mahitaji ya soko ili kuwafikia wateja wengi kwa njia rahisi za kidigitali.

Vilevile alisema wanaendelea na utaratibu wa kuboresha huduma kwa lengo la kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha kunakuwepo na huduma shirikishi za kifedha kwa Watanzania.

"Makubaliano haya ya benki yameifanya benki yetu kuwa miongoni mwa taasisi bora za kibenki hapa nchini, tumeongeza wigo wa kuwafikia wateja wetu ambapo mpaka sasa tumewafikia zaidi ya wateja 200,000," alisema Mseti.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema makubaliano ya benki hizo mbili yameifanya Benki ya ACB kuwa benki ya kimataifa.

Alisema benki hiyo imekuwa miongoni mwa benki ambazo zinafanya vizuri katika kuwahudumia wananchi kwenye mambo ya kifedha.

# Mfumo ufuatiliaji mazao shambani wazinduliwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MFUMO wa kisasa wa kufuatilia mazao yakiwa shambani mpaka yanaponunuliwa na kwenda kuchakatwa viwandani, umezinduliwa nchini.

Mfumo huo uitwao Solichain umeandaliwa na Shirika la Solidaridad kutoka Uholanzi, ukitumia teknolojia ya brockchain unalenga kuwasaidia wakulima na wanunuzi wa mazao kupanga bei kwa kuzingatia gharama za uzalishaji.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mfumo huo jijini Mbeya, Meneja wa Shirika la Solidaridad nchini, Godlove Nderino alisema mfumo huo umelenga kuwasaidia wakulima na wanunuzi wa mazao nchini kufuatilia mwenendo wa mazao yao tangu yanapoanza kuzalishwa mpaka yanapochakatwa kiwandani.

"Mfumo huu utawasaidia wanunuzi na wakulima kujua nani kazalisha mazao, mahali yalipozalishwa, hahitaji na gharama za uzalishaji hali ambayo itasaidia pande zote mbili kupanga bei ambayo itawanufaisha wote," alisema Nderino.

Alisema kuwa kwa kuanzia mfumo huo utaanza kutumika kwenye zao la Kahawa kwa wakulima na wanunuzi wa mikoa ya Nyanda za Juu kusini.

Mwakilishi wa Wizara ya Kilimo kwenye uzinduzi wa mfumo huo, Dainess Mtei alisema mfumo huo umeingia nchini kwa mara ya kwanza na kwamba ni mzuri na unafaa pia kutumiwa na wakulima wa mazao mengine.

"Mfumo huu una manufaa makubwa kwa wakulima wetu na kwenye sekta nzima ya kilimo, kutokana na faida zake unapaswa pia kutumika kwenye mazao mengine hususani yale ambayo yanaendeleshwa kwa mfumo wa vyama vya ushirika kama vile chai, pamba na parachichi," alisema Dainess

Alisema kuwa anaamini mfumo huo unaweza kusaidia kupunguza kero nyingi za wakulima na kuwainua kiuchumi kwa kuwa itakuwa siyo rahisi mkulima kupata hasara kutokana na mazao yake kununuliwa kwa bei ya chini ikilinganishwa na gharama zilizotumika kwenye uzalishaji.

Kwa upande wake Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Songwe, Pascal Kulanga alisema kuwa mfumo huo una faida kubwa kuanzia kwa wakulima, wanunuzi wa mazao na taifa kwa ujumla.

Alisema kuwa mfumo huo utaepusha hasara waliyokuwa wakiipata wakulima kutokana na kutumia gharama kubwa pembejeo wakati wa uzalishaji, lakini wanapouza mazao yao bei hupangwa na wanunuzi bila kujali gharama zilizotumiwa na wakulima.

Baadhi ya wadau wa kahawa Nyanda za Juu Kusini walisema kuwa mfumo huo umekuja kwa muda muafaka ambapo walikuma walikuwa wamekaribia kukata tamaa ya kulima kahawa kutokana na kuuza mazao yao kwa bei ndogo zisizoendana na gharama za kilimo cha zao hilo.

# Dk. Mwinyi ahimiza umoja, amani, mshikamano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi amesema Zanzibar, inahitaji kuzidi kuendelezwa kwa hali ya umoja na mshikamano kwa sababu ndiyo siri kubwa ya mafanikio yaliyopo katika kuimarisha amani, ustawi wa uchumi na kukuza maendeleo ya jamii.

Aliyasema hayo jana katika hotuba yake ya Baraza la Iddi iliyosomwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman.

Alisema Zanzibar imefikia kuwa nchi ya amani kutokana na misingi ya uongozi bora iliyowekwa na viongozi wa awamu zote zilizopita na uwezo wake Mwenyezi Mungu.

"Kila mmoja wetu ana wajibu wa kufurahia baraka alizotupa Mwenyezi Mungu na kufanya kila jitihada ili tuilinde hali ya neema na kheri"alisema.

Dk. Mwinyi alisema ni lazima kuhakikisha kwamba hakuna hata mmoja atakayekuwa ni chanzo cha kuvurugika kwa amani katika nchi kwa visingizio vya harakati za kidini, kisiasa na nyingine.

"Tuiendeleze sifa ya nchi yetu kuwa ni nchi ya amani kwa kujiepusha na mifarakano na mizozo isiyokuwa na faida yoyote"alisema. Aidha, alisema sikukuu ni furaha lakini kila sikukuu huwa na sababu zake, hivyo, aliwataka wananchi kutumia sikukuu kwa kufanya mambo mema yenye mnasaba wa kuonesha furaha.

Alisema miongoni mwa mambo mema ya kuyatekeleza ni lile la kuchinja mnyama kwa matumizi ya familia na kuwapa sehemu ya mnyama marafiki, yatima na watu wingine hasa wasio na uwezo.

Dk. Mwinyi alsiema wananchi wa Zanzibar wanasherehekea sikukuu hiyo wakati nchi ipo katika harakati za matengenezo makubwa ya barabara za mjini na maeneo mingine na hali hiyo inaweza kusababisha hali ya usumbufu katika upatikanaji wa huduma ikiwemo usafiri barabarani.

Hivyo, aliziagiza taasisi za serikali zikiwemo Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na Shirika la Umeme (ZECO) kufanya kazi kwa karibu na makandarasi wanaotekeleza ujenzi wa barabara ili kupunguza athari zinazotokana na harakati za ujenzi wa barabara zinazoendelea.

"Kadhalika, niwaombe wananchi kuwa wastahamilivu kutokana na athari zinazotokana na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara kwa kuamini kuwa hali hii ni ya mpito na ina manufaa makubwa na faida nyingi kwetu sote baada ya kukamilika kwake"alisema.

Alisema serikali inaendelea kuwasimamia makandarasi ili kuhakikisha kazi yao inamalizika kwa muda kulingana na mikataba na miradi hiyo ya ujenzi inakuwa na viwango bora na itakayodumu kwa muda mrefu.




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akizungunza katika Baraza la Eid Al Adha, mjini Zanzibar jana. **PICHA: OMKR**

# Wanandoa epukeni talaka, kuwaokoa watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANDOA wameshauriwa kujitahidi kuzichunga ndoa zao na kupunguza wimbi la talaka zinazosababisha kusambaratika kwa watoto wao.

Ushauri huo umetolewa na wasaidizi wa sheria wakati wakiwasilisha mrejesho wa vikundi kazi vya wilaya za Unguja, katika kipindi cha miezi sita.

Aziza Simai miongoni mwa wasaidizi hao wa sheria alisema miongoni mwa sababu zinazochangia kuongezeka kwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto ni kuvunjika kwa ndoa.

Akieleza changamoto zilizopo katika mapambano ya vitendo vya udhalilishaji muhali ambao bado upo katika jamii na kesi hizo kuzimaliza katika ngazi za familia.

Aidh,a alisema kumekuwepo kwa malalamiko mengi kwa baadhi ya wanasheria juu ya kushirikiana na wazazi kuwashusha umri watuhumiwa wa kesi za udhalilishaji jambo ambalo linafanyika kwa pande zote mbili na kusababisha kupoteza vielelezo vya ushahidi wa kesi.

Alisema katika Wilaya ya Magharib Unguja, matukio 71 wameyaibua kufuatia utoaji wa elimu kwenye wilaya hiyo kuanzia kupindi cha Januari hadi Juni mwaka huu.

Naye Mkuu wa Divisheni ya Jinsia kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Halima Abdurahman Omar aliwataka wasaidizi wa sheria kuendelea kupambana na matukio hayo ya udhalilishaji ambayo yakiathiri jamii ambayo ni nguvu kazi ya taifa.

Akifungua mkutano huo Mkurugenzi Idara ya Jinsia na Watoto, Siti Abbas Ali aliwapongeza wasaidizi wa sheria kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kuhakikisha wanawasaidia wanawake na watoto katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Pia, aliwashauri wasaidizi hao kujitahidi kuibua mbinu mpya katika kipindi kijacho cha Julai /Septemba ili kumaliza au kutomeza vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia.

## Serikali yatangaza kiama watakaochezea mifumo ya kodi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inakwenda kutekeleza bajeti ya serikali kwa mwaka 2023-2024 kwa kishindo, huku ikitoa onyo kali kwa watendaji watakaochezea mifumo ya malipo na kuikosesha serikali mapato, kwamba watachukuliwa hatua za kisheria.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Dk.Saada Mkuya Salum wakati akizungumza na watendaji wa wizara yake kufuatia serikali kupitisha bajeti ya fedha kwa mwaka 2023-2024.

Alisema serikali imeweka malengo ya kutumia Sh.trioni 2.8 ambazo zinatakiwa zitoke katika vyanzo vya mapato yanayokusanywa na taasisi mbalimbali.

Dk. Mkuya alisema serikali tayari imetengeneza mifumo wa ukusanyaji mapato pamoja na manunuzi pamoja na utoaji wa risiti kwa ajili ya kufanya makusanyo makubwa ya fedha.

Aliitaja mifumo ambayo ndiyo inayotumika kwa sasa ikiwemo mfumo wa manunuzi, mfumo wa ukusanyaji wa ZIDRAS na ule wa ZAN Malipo ambayo imekubalika kutumika.

Waziri huyo alisema kwa upande wa utoaji wa risiti VFMs ndiyo utakaotumika kwa ajili ya wafanyabiashara. "Hiyo ndiyo mifumo ambayo tumekubaliana nayo itumike katika kufanya manunuzi na ukusanyaji pamoja na kutoa risiti za kielektroniki ambayo watendaji wote katika taasisi za fedha wanatakiwa kuitumia kikamilifu katika utekelezaji wao wa kufanya ukusanyaji wa kodi,"alisema.".

Aidha alisema serikali itaendelea kutumia mifumo ya kielektroniki ya ufuatiliaji na kufanya tathmini katika kuziba mianya inayotokana na upotevu wa fedha za serikali.

Alisema mikakati ya serikali katika mwelekeo wa utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2023-2024 ni kuziba mianya ya kodi pamoja na kupunguza na kuondosha misamaha ya kodi ambayo baadhi yake imekuwa ikiikosesha serikali mapato makubwa.

"Huo ndiyo mwelekeo wetu kutumia kikamilifu mufumo yote ya ukusanyaji wa kodi pamoja na kupunguza na kuondosha misamaha ya kodi ambayo baadhi yake tumebaini ikilikosesha taifa mapato,"alisema. Naibu Waziri wa wizara hiyo, Ali Suleiman Ameir aliwataka watendaji wa ZRA kujipanga zaidi kuhakikisha wanayatimiza malengo yaliyowekwa ya ukusanyaji wa Sh. bilioni 675.60 katika mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema malengo hayo yatafikiwa endapo watajipanga kwa kuongeza ufanisi ikiwemo ufuatiliaji na kuziba mianya yote ambayo hupoteza mapato ya serikali.

# SIKUKUU YA EID AL ADHA KATIKA PICHA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Balozi wa Nigeria nchini, Dk. Hamisu Umar Takalmawa, wakati alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Swala ya Eid- Adha na Baraza la Eid-Adha Kitaifa kwenye Msikiti wa Mfalme wa Morocco Muhammad VI, Kinondoni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**




Wanawake wa dini ya kiislamu wakishiriki swala ya Eid Al Adha katika viwanja vya Msikiti Mkuu wa Gadafi, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Mwanahamisi Mumkunda (kulia), akikabidhi mfuko wenye nyama kwa Mariam Selemani, iliyotolewa na Taasisi ya Muslim World League kwa ajili ya Sikukuu ya Eid Al Adha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wananchi wakichuna mbuzi katika eneo la Kizota, jijini Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya Sikukuu ya Eid Al Adha ambayo huambatana na kuchinja wanyama baada ya swala. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**




Waumini wa dini ya Kiislam wakishiriki swala ya Eid Al Adha, katika Msikiti Mkuu wa Ijumaa. wilayani Muheza mkoani Tanga jana. Katikati ni Diwani mstaafu wa kata ya Mbaramo, Makame Seif na (wapili kulia), mfanyabiashara Hassan Elisi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Waumini wa dini ya Kiislam wakishiriki swala ya Eid Al Adha nje ya Msikiti Mkuu wa Ijumaa, wilayani Muheza, mkoani Tanga jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Maajabu ya Titan, Titanic na vyombo vya majini yakikumbukwa baada ya miaka 110





Taswira mbili za nyambizi ya Titan, kabla na baada ya kuanza safari chini ya bahari. **PICHA: BBC**

**Na Christina Mwakangale**

NYAMBIZI ya Titan iliyozama Jumapili iliyopita, Juni 18, mwaka huu, imezama eneo ambako pia meli ya kifahari ya Titanic ilizama miaka takribani 113 iliyopita, ikiwa imeabiri abiria matajiri na wakitokea nchini Marekani.

Kisa cha kuzama kwa nyambizi ya Titan pamoja na Titanic, kina uhusiano kwa maana ya eneo ilikozamia, bahari moja ya Atlantiki, ikibeba mabilionea na kuzama saa chache tu baada ya safari.

Pia, uhusiano wa nyambizi hiyo ni kwamba, Ofisa Mtendaji Mkuu na Mwanzilishi wa kampuni ya OceanGate, Stockton Rush (61), aliyefariki katika nyambizi hiyo, alimuoa kitukuu cha Isidor na mkewe Ida Straus, ambao nao walifia majini baada ya ajali ya meli ya Titanic.

Ofisa Mtendaji Mkuu huyo na Mwanzilishi wa kampuni ya OceanGate, Rush, ni miongoni mwa watano waliosafiri na nyambizi ya Titan, umbali wa inayomilikiwa na kampuni yake, iliyozama Juni 18, mwaka huu, saa chache tangu ianze safari, ikipoteza mawasiliano.

Wengine waliokuwamo, Mvumbuzi wa Uingereza Hamish Harding (58), Shahzada Dawood (48) na mwanawe, Suleman Dawood (19) na mpiga mbizi Mfaransa Paul-Henry Nargeolet (77). Wote walifariki.

Ukirejea meli ya Titanic, nayo ilizama saa chache tangu iache ufukwe wa bahari hiyo, April 14, mwaka 1912 ikibeba abiria wapatao 2,000 wengi wao wakiwa matajiri, kati yao 1,500 walifariki dunia hadi sasa mabaki ya meli hiyo kubwa ya abiria duniani, yamo baharini ikiwa ni sehemu ya utalii.

Kutokana na umaarufu wa meli hiyo kubwa, Desemba 19 mwaka 1997, iliandaliwa filamu iliyojipatia umaarufu duniani na kuwa kati ya filamu zilizotuzwa tuzo zipatazo 90 ikiwamo ya Grammy na kutazamwa na watu wengi duniani, iliyoandaliwa na James Cameroon.

Akifanyiwa mahojiano na televisheni ya BBC ya nchini Uingereza, saa chache baada ya nyambizi ya Titan kuzama, Cameroon anasema: " Haukuwa uchaguzi sahihi kwa kampuni ya OceanGate kufanya safari ya kitalii katika eneo hilo lenye kina cha maji zipatazo mita 3,800 bila kuwahusisha wataalamu wa masuala ya baharini."

Cameroon anasema kabla ya safari walipaswa kufanya utafiti kwa kuwa eneo hilo bado ni hatari baada ya ajali, kutokana na kina cha bahari eneo hilo.

"Kwa eneo hilo lilivyo ilitakiwa kizazi hiki cha karne ya 21 kuchukua tahadhari. OceanGate wana wataalamu wa masuala ya bahari. Ni uchaguzi mbaya naweza kusema hivyo na sio rekodi," anasema Cameroon.

**SAFARI YA TITAN**

Nyambizi ya Titan iliyozama ikiwa na watu watano, Juni 18, mwaka huu, ilikuwa inakwenda kutalii sehemu yalikobaki mabaki ya meli maarufu ya kitalii ya Titanic.

Thamani ya safari hiyo ya siku nane, ilipangwa kwa atakayelipia tiketi ya dola za kimarekani 250,000. Katika safari hiyo kwenda kuzuru masalia ya Titanic, huonekana kwa kwenda umbali wa mita 3,800 chini ya bahari ya Atlantiki.

Kati ya abiria watano katika chombo hicho alikuwamo mfanyabiashara bilionea mzaliwa wa Pakistan, Shahzada Dawood na mtoto wake Suleiman Dawood.

Wengine ni mfanyabiashara bilionea raia wa Uingereza, Hamish Hardin, mvumbuzi wa Kifaransa Paul Henri Nargelet na Mkurugenzi mkuu wa kampuni ya OceanGate, iliyohusika na safari hiyo, Rush.

Kabla ya kuanza safari, Harmish Harding aliandika kupitia mtandao wa kijamii, anajivunia kutangaza atakuwa sehemu ya safari ya kuelekea katika mabaki ya Titanic. Aliandika : "Hii itakuwa safari ya mwisho kwa mwaka huu, kwenda Newfoundland, kwa sababu msimu huu baridi imekuwa kali kwa mara ya kwanza tangu kupita kipindi cha miaka 40."

Lakini baada ya safari hiyo chini ya saa tatu, Walinzi wa pwani ya Marekani, wakidai mawasiliano na nyambizi yamepotea. Walinzi wa pwani ya Marekani, pia siku iliyofuata Juni 20, mwaka huu, siku ya Jumatatu usiku, nyambizi hiyo, walisema nyambizi hiyo itakuwa na oksijeni ya kuwawezesha kuishi waliomo kwenye Titan, kwa siku nne.

"Tunakadiria kutoka sasa, kutakuwa na masaa 70 hadi 96 kukamilisha operesheni ya utafutaji, walisema walinzi hao wakidai eneo la operesheni ni gumu, kwa sababu kuna vikwazo vingi wanakutana navyo.

Kwa mujibu wa tovuti ya kampuni ya OceanGate, kulikuwa na mipango ya kufanya safari hizo mara mbili kwa mwaka, kuanzia mwaka ujao, yaani 2024.

Nyambizi hiyo ndogo ilibeba rubani na abiria watatu walionunua tiketi. Mbali na hao, mtaalamu pia yumo katika nyambizi. Safari yao ilianza eneo la St. John katika kisiwa cha Newfoundland, Canada.

Uzito wa nyambizi ni kilogramu 10,432 ikiwa na uwezo wa kwenda umbali wa futi 13,100. Ikiwa na oksijeni ya kudumu saa 96 katika nyambizi.

Hadi jana, vyombo vya habari vya kimataifa vilisema vipande kutoka kwenye nyambizi hiyo ndogo, ambayo ilizama eneo ilikozama meli Titanic, viliokotwa huko St John's, Canada.

Pia, yamepatikana mabaki ya binadamu kutoka nyambizi Titan, Jeshi la Walinzi wa Pwani la Marekani, linasema.

Maofisa hao wanasema fremu ya kutua na kifuniko cha nyuma ni kati ya vifusi vilivyopatikana.

Bodi ya Uchunguzi wa Majini ya Walinzi wa Pwani (MBI) itasafirisha ushahidi hadi bandari ya Marekani kwa uchambuzi na uchunguzi zaidi.

Mwenyekiti wa MBI Kapteni Jason Neubauer anasema katika taarifa kwamba "bado kuna kazi kubwa ya kufanywa kuelewa mambo yaliyosababisha kupotea kwa ajali ya Titan na kusaidia kuhakikisha ajali kama hiyo haitokei tena."

"Haya ni mazingira ya kipekee huko chini kwenye sakafu ya bahari," Mlinzi wa Pwani, Adm John Mauger amesema, muda mfupi baada ya kupotea kwa nyambizi na kuthibitishwa.

Kapteni Neubauer anasema wakati huo wachunguzi watachukua "tahadhari zote" ikiwa watagundua mabaki ya binadamu na kwamba uchunguzi huo unaweza kujumuisha kusikilizwa rasmi kwa ushahidi wa mashahidi.

Walinzi wa pwani wanasema, vipande vitano vikubwa vya meli hiyo ndogo vimepatikana kwenye uwanja mkubwa wa uchafu karibu na ukingo wa meli ya Titanic.

Mabaki ya Titanic yapatikana kilomita 700 Kusini mwa kisiwa cha Newfoundland ambalo pia inafanyika operesheni ya kusaka masalia ya Titan, huko Boston, Massachusetts, Marekani.

**STOCKTON ALIMUOA KITUKUU CHA WALIOZAMA NA TITANIC**

Stockton Rush, mwanzilishi na Mkurugenzi mkuu wa OceanGate, ambaye amefia majini, aliingoza nyambizi hiyo.

Rush, alimuoa Wendy, kitukuu cha Isidor and Ida Straus, ambao walizama miaka 113 wakiwa kati ya abiria 2,000 waliokuwamo kwenye meli ya Titanic. Ida ambaye ni miongoni mwa Wanawake waliopatiwa jaketi la kujiokoa boya' (life jacket), alilivua na kumpa mmoja wa wafanyakazi ndani ya meli, mwanamke, na yeye kusalia na mumewe wafe wote.

Mkewe Isdori, Ida, aliamua kusalia na mumewe baada ya ajali ya Titanic na kukataa kuokolewa na meli za uokoaji kwa kuwa sharti la waokoaji lilikuwa kipaumbele ni kuwaokoa wanawake na watoto, kwa kuwa vyombo vya uokoaji vilikuwa vichache. Uhalisia wa tukio hilo umeigizwa kwenye filamu ya Titanic, iliyoongozwa na Cameroon.

**CAMEROON NI NANI?**

Cameroon aliingoza filamu ya Titanic na kuitoa rasmi mwaka 1997 ikiwa ni igizo la tukio la kweli la kuzama kwa meli hiyo, lililotokea mwaka 1912.

Waigizaji wakuu wakiwa, Kate Winslet na Leonardo DiCaprio. Cameroon anasema kisa cha filamu walikipatia kutoka kwa mmoja wa abiria aliyeabiri Titanic, baada ya kumpa simulizi.

Gloria Stuart aliyeigiza kama Rose Dawson Calvert, akiwa na miaka 100 alitoa simulizi ya meli hiyo.

Filamu hiyo iligharimu dola za kimarekani milioni 200.

**UHALISIA MELI YA TITANIC**

Meli ya Titanic ilizama wakati wa safari yake ya kwanza kutoka New York 1912. Ilikuwa ni meli kubwa zaidi kwa wakati huo. Kati ya abiria na wafanyakazi wa meli 2,200, zaidi ya 1,500 walikufa. Mabaki ya meli yaligundulika kwa mara ya kwanza 1985.

Iligongana na mwamba wa barafu wakati wa usiku wa giza nene. Wakati huo abiria wengi walikuwa wamo usingizini.

***Imeandiliwa kwa msaada wa vyanzo tofauti mtandaoni**

# YANGA YAPIGWA FAINI, ALIYEMPIGA KOCHA WA MBEYA CITY AFUNGIWA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU za Yanga na Mbeya City zimepigwa faini kutokana na makosa mbalimbali wakati wa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara baina yao iliyochezwa Juni 6 kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya na kutoka sare ya mabao 3-3.

Mbali na hilo, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), Kocha wa magolikipa wa Mashujaa FC, Shomari Ndizi, amefungiwa kushiriki michuano yote inayosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF) kwa msimu mzima ujao wa 2023/24 kwa kosa la kumpiga ngumi usoni kocha wa Mbeya City, Abdallah Mubiru katika mechi ya 'Play off' kati ya timu hizo mbili iliyochezwa Uwanja wa Sokoine Mbeya Juni 23 mwaka huu.

Ndizi wakati akirejea kwenye benchi lake kutoka kushangilia bao pekee la timu yake alionyesha kitendo cha ajabu baada ya kuonekana akimpiga ngumi ya uso Mubiru aliyekuwa amesimama kwenye benchi lake

"Adhabu hizi zote zimetolewa na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) katika kikao chake kilichokaa Juni 27 mwaka huu kwa asjili ya kupitia mwenendo mbalimbali na matukio ya ligi," ilisema sehemu ya taarifa hiyo ya bodi ya ligi.

Kwenye adhabu hizo, Mbeya City imetozwa faini nyingi kuliko Yanga kwa kutakiwa kutoa Sh. Milioni 2.5, huku Wanajwangani hao wakitakiwa kulipa Sh. Milioni 1.

Yanga imepigwa faini hiyo kutokana na mashabiki wake kuwarushia chupa walinzi wa uwanjani wakati mechi ikiendelea.

katika mechi hiyo hiyo ambayo Mbeya City ilifunga mabao matatu na Yanga ikarudisha yote, wenyeji wametozwa faini ya Sh, 500,000 kwa kosa la watoto waokota mipira kuchelewesha kwa makusudi kurejesha mipira uwanjani kama hila ya kupoteza muda baada ya wenyeji kufunga bao la tatu dhidi ya Yanga, Pia imetozwa faini ya Sh. Milioni moja baada ya mashabiki wake kuwarushia chupa wachezaji wa Yanga wakati wanashangilia moja ya mabao waliyofunga katika mchezo huo.

Katika mechi nyingi iliyocheza dhidi KMC, Mbeya City imepigwa faini nyingine ya Sh. Milioni moja kwa kosa la mashabiki wake kuwapiga na kuwasababishia majeraha baadhi ya mashabiki wa KMC, mechi hiyo iliyochezwa Sokoine na Mbeya City kushinda mabao 2-1.



Wachezaji wa timu ya walemavu ya kurusha tufe wakifanya mazoezi ya viungo katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Nusu Fainali U20 kupigwa leo Chamazi

**Na Adam Fungamwango**

NUSU fainali ya Ligi ya Vijana ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), itapigwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex kwa kushuhudia michezo miwili ambapo Kagera Sugar itakabiliana na Geita Gold FC saa 9:00 alasiriwakati Mtibwa Sugar watavaana na wenyeji Azam FC majira ya saa 12:00 jioni.

Timu hizo zinacheza hatua hiyo baada ya kushinda mechi zao za robo fainali juzi, Geita Gold ikiishindilia Mbeya City mabao 2-1, huku Kagera Sugar ikiiondosha Dodoma Jiji mabao 2-0.

Mabingwa Watetezi, Mtibwa Sugar walipata tiketi hiyo kwa kuitwanga Coastal Union mabao 2-0 na Azam FC ikaisasambua Prisons kwa mabao 3-1.

Fainali ya ligi hiyo inatarajiwa kuchezwa Julai 2 kumpata bingwa wa ligi hiyo ya vijana kwa mwaka huu.

Wakati huo huo, nyota wa Tanzania Prisons , Idd Kichindo licha ya timu yake kutolewa kwenye hatua ya robo fainali, bado anaongoza kwa ufungaji mabao mpaka sasa akiwa amepachika mabao matano.

Kichindo anafuatiwa na Zidane Sereli wa Dodoma Jiji, Athumani Makambo wa Mtibwa Sugar na Nicodemas Mtarema wa Geita Gold wenye magoli matatu kila mmoja.

Zidane timu yake imeshatolewa, hivyo wachezaji ambao wanaweza kumnyima Kichindo kiatu cha dhahabu ni Makambo na Mtarema.

## *KMC yajiandaa kutangaza benchi la ufundi*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imesema inajiandaa kulitangaza benchi la ufundi ambalo ndilo litachukua jukumu la kufanya usajili kwa ajili ya msimu ujao wa 2023/14.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala amesema kwa sasa wanaweka mambo sawa ili kila kitu kikamilike na walitangaze benchi lao la ufundi ambalo litakuwa na jukumu la kusajili wachezaji w akuongeza nguvu.

"Tayari kuna wachezaji tumeshazungumza nao, lakini kwa sasa tunaweka mambo sawa kwa ajili ya kulitangaza benchi la ufundi tutakalokuwa nalo msimu wa 2023/24, tukimaliza kila kitu tutawatangazia mashabiki na wapenzi wa KMC na hao ndiyo watakaokuwa na jukumu la kufanya usajili, na sisi tutawaonyesha wachezaji tuliozungumza nao, kama watafaa basi watawachukua," alisema Mwagala. KMC imeponea chupuchupu kushuka daraja na kujikuta inacheza hatua ya 'Play off' dhidi ya Mbeya City kuwania kusalia ligi kuu.

Mechi hizo za Play Off KMC ilikuwa chini ya kocha Jamhuri Kiwhelo 'Julio' ambaye aliichukua timu hiyo ikiwa kwenye hali mbaya katika msimamo wa ligi na aliiongoza kwenye mechi mbili za mwisho na kunusurika kushuka daraja moja kwa moja na kwenda kucheza michezo miwili ya 'Play Off' ambayo walifanikiwa kubaki ligi kuu.

Hivi karibuni, Julio alielezea hatma yake kwenye klabu hiyo hasa baada ya kukamilisha kazi ya kuinusuru KMC kushuka daraja.

"Nilipopewa timu walitaka kunipa mkataba wa miaka miwili, lakini niliwaambia hapana ngoja kwanza tuinusuru timu mambo mengine yatakuja, na kweli tumeinusuru, tumeshaanza mazungumzo ya kubaki kwenye timu vile vile na masuala ya usajili kwa sababu muda unakwenda kuna muda mfupi tu kianze kipindi cha 'pre season', kwa hiyo tunataka tufanye usajili mzuri ili tusiwe wasindikizaji msimu ujao, nina imani nitabaki KMC kwa hili nililolifanya, lakini ikitokea kama kutakuwa na kocha mwingine wamemuona anafaa mimi sina tatizo, ila kwa jinsi tulivyomaliza mechi zetu na tulivyozungumza, wanaonekana bado wana haja na mimi," alisema Julio.

## Kidunda: Njooni muone ninavyopiga mtu

**Na Saada Akida**

BONDIA Seleman Kidunda amewataka mashabiki wa ngumi kujitokeza leo kwenye ukumbi wa Mlimani City kushuhudia akimpiga mpinzani wake Erick Mukadi raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Akizungumza jana muda mfupi baada ya kupima uzito kuelekea kwenye pambano hilo la leo la raundi 10 lisilo la ubingwa, Kidunda, alisema amejiandaa vizuri kwa pambano hilo na kwa saa anasubiri hamasa ya mashabiki watakaojitokeza kwenye ukumbi huo leo.

"Nimefurahi sana kuona watu wengi wamejitokeza katika zoezi la upimaji uzito leo (jana), ombi langu naomba wajitokeze tena kesho (leo) katika Ukumbi wa Mlimani City kunipa hamasa ya kushuhudia burudani nzuri kutoka kwangu, "alisema Kidunda na kuongeza,

"Siwezi kusema nitampiga raundi ya ngapi ila atakavyokuja ndivyo tutampokea, ninachowambia watanzania wajitokeze kwa wingi kwa sababu nimefanya mazoezi ya kutosha, "alisema.

Kwa upande wake Mukadi akizungumzia pambano hilo la leo alisema amekuja Tanzania kwa ajili ya kumpiga Kidunda na sio kucheza ngumi.

"Nimekuja kwa kazi moja tu, kumstaafisha ngumi Kidunda na nitampiga kama ngoma siku ya kesho (leo, kwa sababu nimejipanga vizuri," alisema Mukadi.

Promota wa pambano hilo, Fadhili Maogola alisema mbali ya Kidunda kupanda ulingoni leo pia bondia Mfaume Mfaume atacheza pambano la kimataifa dhidi ya Nkululeko Mhlongo wa Afrika Kusini. .

"Maandalizi yamekamilika leo (jana) wanapima uzito tayari kwa mapambano haya, tunatarajia mapambano yoteb yatakuwa ya upinzani mkubwa kutokana na mabondia wanaocheza kuwa na rekodi nzuri na uwezo," alisema Maogola.

Maogola alitaja mabondia ambao watacheza mapambano ya utangulizi kuwa ni Fadhili Majiha 'Stopper' atakayepanda ulingoni dhidi ya Jamal Kunoga wakati Saleh Kasim atamalizana na Said Bwanga kabla ya Deo Samweli kumvaa Adam Ngange.

Wengine ni Pius Mpenda atapanda ulingoni dhidi ya Simon Tichecha wa Malawi wakati Rama Jonh Cina akitarajia kupigana na Yona Segu, Omary Maulid atapigana na Shaban Kibiriti, Boniface Seguda atapigana na Hamza Mahamoudu huku Herry Rashid akitarajia kumalizana Hussein Pendeza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE SAFI ARSENAL

KIUNGO wa kati wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24 amepewa ruhusa ya kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu katika klabu ya Arsenal wakati wakifanya mazungumzo na West Ham kuhusu makubaliano ya dau la pauni milioni 105. (***Sport***)

### KANE NA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich iko tayari kutoa pauni milioni 80 kujaribu kumsajili mshambuliaji, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, kutoka Tottenham baada ya ombi la awali la pauni milioni 60.2 kwa nahodha huyo kukataliwa. (***Sun***)

### MOYES ATAKA NYOTA

KOCHA wa West Ham, David Moyes anawalenga kiungo wa Everton raia wa Ubelgiji, Amadou Onana mwenye umri wa miaka 21, kiungo wa kati wa Juventus na Uswisi, Denis Zakaria mwenye miaka 26 na mlinzi wa Manchester United, Harry Maguire mwenye miaka 28. (***Mirror***)

### CAICEDO ATAKIWA

KLABU ya Manchester United inatazamiwa kuwasiliana rasmi na Brighton kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21, baada ya kuwasiliana mara ya kwanza wiki hii. (***Sky Sports***)

### MOUNT AWINDWA

MANCHESTER United pia watafanya mazungumzo na Chelsea wiki hii ili kuvunja mvutano kuhusu mkataba wa kiungo wa kati wa England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24.

### VEIGA AFUATILIWA

KIUNGO wa kati wa Hispania, Gabri Veiga mwenye umri wa miaka 21, ambaye ana kipengele cha kutolewa cha euro milioni 40 ameonekana kulengwa na Manchester City, huku Liverpool na Chelsea pia zikimfuatilia mchezaji huyo wa Celta Vigo. (***Fabrizio Romano***)

### SZOBOSZLAI ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL imekutana na wawakilishi wa kiungo wa Hungary mwenye umri wa miaka 22, Dominik Szoboszlai, ambaye ana kipengele cha kutolewa cha euro milini 70 kutoka RB Leipzig. (***Mail***)

### COADY KUTUA WOLVES

KLABU ya Wolves imekubali dau la pauni milioni 7.5 pamoja na pauni milioni 1 kama nyongeza kutoka kwa Leicester City kwa ajili ya kumnunua beki wa England, Conor Coady mwenye miaka 30. (***Express and Star***)

### SADIKI AWANIWA

KLABU ya Burnley imewasilisha ombi la kumnunua beki wa Anderlecht raia wa Ubelgiji, Noah Sadiki mwenye miaka 18. (***Fabrizio Romano***)

### HUDSON-ODOI ATAKIWA FOREST

CHELSEA iko tayari kumwachia winga wa England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 22 kuondoka kwa pauni milioni 15 na Nottingham Forest wanamuwania. (***Nottingham Post***)

### PHILLIPS NA LEEDS

KLABU ya Leeds United inavutiwa na mlinzi wa Liverpool, Nat Phillips mwenye umri wa miaka 26. (***Athletic***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YAMTWAA RASMI HAVERTZ

**LONDON,** England

**Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani amesaini mkataba wa muda mrefu na klabu hiyo akitokea...**

KLABU ya Arsenal imekamilisha usajili wa fowadi, Kai Havertz kutoka Chelsea katika mkataba ambao ESPN iliripoti wiki iliyopita una thamani ya hadi pauni milioni 67.5.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani ametia saini mkataba wa muda mrefu na klabu hiyo ya kaskazini mwa London na anakuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa na Arsenal katika dirisha hili la joto.

**"Kai ni mchezaji wa ubora wa hali ya juu. Ana uwezo mwingi na ni mchezaji mwenye akili. Ataleta nguvu kubwa ya ziada kwenye safu yetu ya kiungo na anafiti aina ya uchezaji wetu," alisema kocha wa Arsenal, Mikel Arteta.**

"Tunamkaribisha Kai na familia yake katika Klabu ya soka ya Arsenal na sote tunafuraha kuanza kufanya kazi naye tutakapoanza mazoezi ya kujiandaa na msimu ujao hivi karibuni."

Havertz amekuwa na wakati mgumu katika klabu ya Chelsea tofauti na alivyokuwa Bayer Leverkusen kabla ya kuhamia klabu hiyo ya Ligi ya England kwa kitita cha pauni milioni 62 mwaka 2020.

Kiwango cha juu cha maisha ya Havertz Chelsea bila shaka ni "Kai ni mchezaji wa ubora wa hali ya juu. Ana uwezo mwingi na ni mchezaji mwenye akili. Ataleta nguvu kubwa ya ziada kwenye safu yetu ya kiungo na anafiti aina ya uchezaji wetu," alisema kocha wa Arsenal, Mikel Arteta.

"Tunamkaribisha Kai na familia yake katika Klabu ya soka ya Arsenal na sote tunafuraha kuanza kufanya kazi naye tutakapoanza mazoezi ya kujiandaa na msimu ujao hivi karibuni."

Havertz amekuwa na wakati mgumu katika klabu ya Chelsea tofauti na alivyokuwa Bayer Leverkusen kabla ya kuhamia klabu hiyo ya Ligi ya England kwa kitita cha pauni milioni 62 mwaka 2020.

Kiwango cha juu cha maisha ya Havertz Chelsea bila shaka ni bao lake la kushinda mechi katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021 dhidi ya Manchester City.

"Inafurahisha sana kwangu kujiunga na klabu hii na kuwa sehemu ya familia ya Arsenal," alisema Havertz.

Havertz amekuwa na wakati mgumu katika klabu ya Chelsea tofauti na alivyokuwa Bayer Leverkusen kabla ya kuhamia klabu hiyo ya Ligi ya England kwa kitita cha pauni milioni 62 mwaka 2020.

Kiwango cha juu cha maisha ya Havertz Chelsea bila shaka ni bao lake la kushinda mechi katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021 dhidi ya Manchester City.

"Inafurahisha sana kwangu kujiunga na klabu hii na kuwa sehemu ya familia ya Arsenal," alisema Havertz.

"Klabu hii ina historia kubwa, na ninatumaini tunaweza kufikia mambo mengi.

"Mawazo katika kikosi cha Arsenal ni ya juu sana na unaweza kuhisi hivyo. Hiyo ilikuwa ni sababu mojawapo kwa nini imekuwa ngumu sana kucheza dhidi ya Arsenal hivi karibuni.

"Lengo ni kushinda mataji na nitatoa kila kitu kufanya hivyo kwa ajili ya mashabiki na kila mtu katika klabu. Sasa ninatazamia kukutana na wachezaji na wafanyakazi wote tutakaporejea kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya."

ESPN iliripoti wiki iliyopita kwamba Havertz aliiarifu Chelsea kwamba hana nia ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo - na kuna uwezekano atacheza mechi yake ya kwanza Arsenal dhidi ya Nottingham Forest Agosti 12.

# Inter Miami yamteua kocha wa Messi

**NEW YORK,** Marekani

KOCHA wa zamani wa Barcelona na Argentina, Gerardo Martino ameteuliwa kuwa kocha mkuu mpya wa Inter Miami.

Muargentina huyo mwenye umri wa miaka 60 anawasili katika klabu ya Ligi Kuu ya soka ya Marekani ambayo mmoja wa wamili wake ni David Beckham baada ya kumfukuza mchezaji wa zamani wa Manchester United, Phil Neville mapema mwezi huu.

Itawakutanisha Martino na Messi, na mshindi wa Kombe la Dunia ambaye amejiunga na timu ya Florida baada ya kuondoka Paris St Germain mwishoni mwa mkataba wake.

Martino, ambaye alimfundisha Messi akiwa na Barcelona na Argentina, alisema katika taarifa yake: "Nina furaha sana kujiunga na klabu kubwa kama Inter Miami na najua kwa pamoja tunaweza kukamilisha mambo mengi makubwa.

"Klabu ina miundombinu muhimu ya kuwa mshindani mkuu katika eneo hili na ninaamini kuwa kwa bidii na kujitolea kwa kila mtu tunaweza kufika huko."

Naye Beckham alisema: "Tata' ni mtu anayeheshimika sana katika mchezo wetu ambaye rekodi yake inajieleza yenyewe.

"Tuna imani kuwa mafanikio yake katika mchezo na uzoefu kama kocha mkuu vitatia moyo timu yetu na kuwasisimua mashabiki wetu na kutarajia kuona mchango mkubwa ndani na nje ya uwanja."

Martino amekuwa mshindi wa Copa America mara mbili akiwa na Argentina na mara moja akiwa na Paraguay, na pia aliisimamia Mexico kushinda Kombe la CONCACAF.





# MOURINHO YAMEMKUTA TENA ITALIA

**ROME,** Italia

KOCHA Mkuu wa AS Roma, Jose Mourinho amefungiwa siku 10 za kuanza kwa msimu wa Serie A kutokana na matamshi aliyotoa kuhusu mwamuzi.

Mourinho ameidhinishwa na mahakama ya kitaifa ya Shirikisho la soka la Italia, FIGC, baada ya kueleza kuwa mwamuzi, Daniele Chiffi kama "refa mbaya zaidi kuwahi kumuona" baada ya mechi ya Roma dhidi ya Monza Mei 3.

Mreno huyo, ambaye pia amewahi kuinoa Chelsea, Manchester United na Tottenham Hotspur, hataruhusiwa kuonekana kwenye chumba cha kubadilishia nguo cha klabu siku za mechi katika siku 10 za kwanza za msimu mpya.

Pia amepigwa faini ya euro 50,000.

Wiki iliyopita Mourinho alifungiwa mechi nne na UEFA kwa kumtusi mwamuzi wa England, Anthony Taylor kwenye fainali ya Ligi ya Europa Mei 31.

Mourinho alimkosoa Taylor katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi na, katika picha za video ambazo baadaye ziliibuka kwenye mitandao ya kijamii, alionekana akimfanyia ishara ya kumtusi Taylor.

Picha za video zilizofuata zilionyesha Taylor akizomewa na mashabiki wenye hasira kwenye Uwanja wa ndege wa Budapest nchini Romania.

UEFA ilijibu hilo katika taarifa mnamo Juni 2, siku hiyo hiyo Mourinho alishtakiwa.

Taarifa hiyo ilisomeka: "UEFA inalaani vikali tabia ya ukatili inayoelekezwa kwa mwamuzi Anthony Taylor na familia yake. Vitendo kama hivyo havikubaliki na vinadhoofisha ari ya kucheza haki na heshima ambayo UEFA inashikilia.

"Waamuzi wana jukumu muhimu katika kuhakikisha uadilifu na usawa wa mchezo, na usalama wao na ustawi wao ni muhimu sana. UEFA inasimama kidete katika kujitolea kwake kuunda mazingira salama na yenye heshima kwa washiriki wote, wakiwemo waamuzi, na haitavumilia aina yoyote ya tabia ya ukatili dhidi yao.

"Tunawaomba wachezaji, makocha na mashabiki wote kukumbatia maadili ya uchezaji michezo, kuwatendea waamuzi kwa utu na heshima, na kuungana nasi katika kudumisha viwango vya juu vya maadili ndani na nje ya uwanja."

# *Mendy aondoka Chelsea atua Al Ahli*

**RIYADH, Saudi** Arabia

GOLIKIPA Edouard Mendy amekamilisha uhamisho kutoka Chelsea kwenda timu ya Saudi Arabia, Al Ahli.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 anakuwa nyota wa hivi karibuni zaidi wa Ligi Kuu ya England kuhamia Saudi Arabia na ataungana na timu hiyo yenye maskani yake Jeddah kabla ya msimu wa 2023-24.


Kipa huyo wa Senegal alianza vyema soka lake la Chelsea baada ya kujiunga na klabu hiyo kutoka Rennais mwaka 2020, na kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na tuzo ya Kipa Bora wa UEFA mwaka wa 2021.

Hata hivyo, Mendy alihangaika sana msimu uliopita na alifanyiwa upasuaji Januari baada ya kuvunjika kidole, na hatimaye kupoteza nafasi yake ya kuwa kipa namba 1 mbele ya Kepa Arrizabalaga.

Al Ahli ilishinda taji la Ligi Daraja la Kwanza la Saudi msimu uliopita na kupata nafasi ya kurudi kwenye Ligi ya Saudi Pro League kwa msimu wa 2023-24.

Al Ahli ni moja kati ya klabu nne, pamoja na Al Hilal, Al Ittihad na Al Nassr, ambazo zilichukuliwa chini ya umiliki wa wamiliki wa Newcastle United, Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia (PIF) mapema mwezi huu kama sehemu ya kile kinachoitwa "Mradi wa Uwekezaji na Ubinafsishaji wa Klabu za Michezo."

Klabu za Saudia zimejihusisha na mkakati mkali wa kusajili wachezaji msimu huu, na kutoa mikataba minono kwa baadhi ya wachezaji wenye majina makubwa katika mchezo huo -- Karim Benzema amejiunga na Al Ittihad huku wachezaji wenzake wa zamani na Mendy, N'Golo Kante na Kalidou Koulibaly pia wakihamia Saudi Pro League.



# SINGIDA FOUNTAIN GATE KUWEKA KAMBI TUNISIA

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Singida Fountain Gate imeanza kufanya usajili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao na imepanga kwenda kuweka kambi nchini Tunisia kujiandaa na msimu mpya Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

Ofisa habari wa klabu hiyo alisema jana kuwa watakwenda kuweka kambi ya 'Pre Season' baada ya kupokea mwaliko wa klabu ya US Monastir ya nchini humo.

"Kwa sasa kamati yetu ipo kazini, inafanya usajili na huwa haikosei, tumefanikiwa msimu uliopita kufanya usajili mzuri ukatupa matokeo mazuri, mpango wetu ni kusajili wachezaji wakubwa na wazoefu wa kutufikisha kwenye malengo, kamati inafanya usajili kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi ambayo yalishawasilishwa kwa uongozi," alisema Massanza na kuongeza,

"Tunatarajia kwenda kuweka kambi Tunisia baada ya kupata mualiko huko, taratibu nyingine zinaendelea mambo yatakapokuwa sawa tutawafahamisha kambi hiyo itakuwa ya muda gani, lakini naweza kuthibitisha kuna mipango hiyo ya kwenda Tunisia," alisema Massanza

**Alisema kuwa tayari wameshawaongezea mikataba wachezaji Bruno Gomes, Yusuph Magoma, na Aziz Andambwile ambao wataendelea kuwa kwenye kikosi hicho hadi 2025.**

"Kwa sababu kuna wachezaji wametufikisha hapa, basi tumeona tuwabakishe na unaona usajili wa wale wote tunaowahitaji kuwabakisha unaendelea na mipango ikienda vizuri kambi yetu tutaweka nchini Tunisia na hii ni ofa tuliyoipata kutoka kwenye klabu ya US Monastir, panapo majaliwa tutaelekea huko kwa ajili ya 'pre seasons', maandalizi yote tayari tunachosubiri ni tarehe rasmi," alisema.

Singida Fountaine Gate iliingia makubalino ya ushirikiano mwezi Machi mwaka huu, wakati US Monastir ilipokuja kucheza mechi ya makundi ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika dhidi ya Yanga.



Wachezaji wa timu ya wanawake ya Ilala Queens, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Uongozi Azam kushusha 'chuma' kingine*

Na Saada Akida

BAADA ya kufanikiwa kusajili nyota wawili wapya, Uongozi wa Azam FC, umesema sasa uko katika mchakato wa kukamilisha usajili wa beki wa kushoto kutoka nchini Cameroon kuja kuchukua nafasi ya Bruce Kangwa aliyepewa mkono wa kwa kheri.

Azam FC tayari wametangaza nyota wawili ambao wamekamilisha usajili wao akiwemo Feisal Salum 'Fei Toto' na kiungo Djibril Sillah anayetarajiwa kutua nchini leo kwa ajili ya kusaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia timu hiyo msimu ujao.

Azam FC juzi iliweka wazi kiungo huyo kutoka Raja Casablanca anakuja kuongeza nguvu kwenye kikosi hicho ambacho kimekosa ubingwa msimu wa 2022/23.

Akizungumza na Nipashe jana, Afisa habari wa klabu hiyo , Hashim Ibwe alisema baada ya kukamilisha usajili wa kiungo huyo sasa wako kwenye hatua za mwisho kumalizana na beki wa kushoto kutoka timu ya taifa ya Cameroon ambayo alicheza CHAN.

Alisema wanatengemea kusajili wachezaji wawili wa kigeni na wamejipanga vizuri kufanya usajili mzuri na wenye malengo na kuhakikisha wanakuwa tishio kwenye kuwania mataji yote msimu ujao.

"Tumefanya usajili mzuri na mashabiki wa Azam FC msimu huu watajipiga kifua kwani tumejiimarisha kwa michuano yote iliyopo mbele yetu ikiwemo Ligi Kuu Tanzania, Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu (FA) pamoja na kombe la Shirikisho Afrika," alisema Ibwe.

## Yanga yakana kufungiwa usajili

INATOKA UK 24

Alisema kocha huyo ataamua nani wa kumsaidia kwenye kazi yake kwa maana ya makocha wake wasaidizi lakini pia watakambidhi ripoti iliyoachwa na kocha Nabi.

"Baada ya kukabidhiwa ofisi na kupewa ripoti iliyoachwa na Nabi yeye sasa ndio ataamua nini cha kufanya, niwahakikishie mashabiki wetu, msimu ujao mwendo ni ule ule tu," alisema Kamwe.

## Simba SC yamng'ang'ania Che Fondoh Malone

INATOKA UK 24

chao kwa msimu ujao wa 2023/24.

"Kuanzia Jumatatu Wanasimba wataanza kuwaona wachezaji wetu wapya tuliokamilisha usajili wao, nasisitiza kila mchezaji tutakayemtaka tutamsajili, wanasimba jumatatu waanze kufuatilia mitandao yetu," alisema Ahmed.

Katika hatua nyingine, Ahmed alisema kocha wao Robertinho ameomba wiki tano za maandalizi mara baada ya kukamilisha usajili wa wachezaji anaowahitaji.

Alisema wiki hizo tano kocha Robertuinho atazitumia kuandaa timu kwa ajili ya msimu mpya wa ligi na mashindano mengine ya kimataifa.


Alisema kikosi cha timu hiyo kinatarajia kwenda kuweka kambi nchini Uturuki kujiandaa na msimu mpya. Msimu uliopita Simba ilienda kuweka kambi nchini Misri.



Michezo

Nipashe

Ijumaa Juni 30, 2023




Arsenal yamtwaa rasmi Havertz UK. 21

# Yanga yakana kufungiwa usajili

●●● Uongozi umesema haujapokea taarifa hiyo zaidi ya kutakiwa kumlipa kocha wao wa zamani, wawatoa hofu mashabiki..

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema licha ya kusikia kwenye mitandao taarifa ya kufungiwa kusajili, wao bado hawajapata barua rasmi na kuwataka mashabiki wa timu hiyo kutokuwa na hofu na taarifa hizo zilizosambaa mitandaoni.

**Tangu juzi kumeibuka taarifa zinazoeleza Yanga kufungiwa kusajili mpaka pale watakampomlipa aliyekuwa kocha wao Luc Eymael raia wa Ubelgiji anayeidai klabu hiyo Sh milioni 354 baada ya ku vunjiwa mkataba wake Julai 20, 2020.**

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe alikiri kuwa wamepokea barua kutoka FIFA inayowasisitiza kumlipa kocha huyo haki yake.

"Sisi Yanga tunashangaa hizi taarifa za kufungiwa zinatoka wapi, ni kweli kocha Eymael anaidai Yanga na barua ya FIFA ambayo imetufikia imetusisitiza kumlipa, hakuna sehemu imeandika kuwa tumefungiwa," alisema Kamwe.

Kamwe amewataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuzipuuzia taarifa hizo kwani si kweli kuwa wamefungiwa.

Alisema ni kweli wanadaiwa na kocha huyo na uongozi chini ya Rais Hersi Said umeanza utaratibu wa kumlipa.

"Hilo suala la kufungiwa usajili sio kweli, lakini nikiri kweli kocha huyo anatudai na nina imani mazungumzo ya ndani yanaendelea kati ya viongozi na kocha huyo na baada ya muda jambo hili litamalizika," alisema Kamwe.

Alisema mashabiki na wanachama wa klabu hiyo wafuatilie na kuziamini taarifa zinazotolewa na uongozi wa timu hiyo kupitia mitandao ya klabu na mahojiano wanayofanya.

Katika hatua nyingine, Kamwe alisema kocha mpya wa klabu hiyo, Miguel Gamond aliyechukua mikoba ya Nasreddine Nabi, anatarajiwa kuwasili nchini wiki ijayo.

Kocha huyo baada ya kuwasili nchini atasaini mkataba wa kuitumikia timu hiyo.

"Kocha akishawasili na kumalizana na uongozi, sasa ndio rasmi tutakuwa tunaanza mikakati yetu kuelekea msimu ujao, tunataka kuendeleza maumivu kwa wapinzani wetu kuanzia pale tulipoishia," alisema Kamwe.

INAENDELEA UK 23



Luc Eymael

## Simba SC yamng'ang'ania Che Fondoh Malone

**Na Saada Akida**

KLABU ya Simba imekana kumkosa beki raia wa Cameroon Che Fondoh Malone wanayemuwania na kudai bado mazungumzo yanaendelea.

Beki huyo anayechezea klabu ya CotonSport awali alikuwa akihusishwa kutaka kusajiliwa na Simba lakini baadae zilisambaa taarifa kuwa wameshindwana.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally alisema timu inayomilikiwa na mwekezaji Mohammed Dewji haishindwi kumsajili mchezaji yeyote wanayemuhitaji kulingana na thamani ya nyota huyo.

Alisema sio kweli kuwa wameshindwa kumsajili mchezaji huyo, bado viongozi wapo kwenye mazungumzo na wakimuhitaji wana uwezo wa kumsajili kutokana na bajeti ya usajili waliyoitenga msimu huu.

"Kama kweli huyo beki anatakiwa au mchezaji yeyote basi Simba haishindwi kumnunua, timu inayomilikiwa na Mo Dewji hatushindwi kumpata, hatusajili wachezaji waliokuwa huru bali tunaenda kuwanunua kutoka ndani ya klabu zao, mapendekezo ya usajili ni kupata beki kuja kusaidiana na Joash Onyango na Henock Inonga kwa msimu ujao wa mashindano, lazima tufanye usajili bora kulingana na mahitaji yetu na mashindano tunayoenda kushiriki," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa katika suala la fedha kwao sio kikwazo cha kufanya usajili, kuna watu waliopewa jukumu la usajili na kufanya kazi kulingana na mahitaji ya Kocha wao Roberto Oliviera 'Robertinho', na usajili wao sio wa wachezaji huru bali wananunua.

Alisema wanatarajia kutangaza rasmi usajili mpya jumatatu ya wiki ijayo kwa wale waliokamilisha masuala ya usajili kwa kutumikia kikosi

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >